African Journal of Advanced Social Sciences

AJASS




Open Access

Check for updates

RESEARCH ARTICLE **Section:** *Literature, Linguistics & Criticism*

# Mitazamo ya Distopia Katika Riwaya Teule za Kiswahili

**Martha Nyangweso Syekei[1]. Carren Nyandiba[2], & Silas Owala[3]**

[1&2]Chuo Kikuu cha Rongo
[3]Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Lugha, Fasihi na Utamaduni, Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

## IKISIRI

Fasihi kama kioo cha jamii, huelimisha, huhifadhi tamaduni za jamii na pia kuadilisha. Utafiti huu wetu ulifaidi kutoka kipengele cha fani kwa kuhakiki mtindo na mitazamo. Daistopia ni jamii iliyochorwa na mwandishi wa kazi ya fasihi andishi na sifa kuu ya jamii hii lengwa ni kutozingatia maadili. Utafiti huu ulihakiki utanzu wa riwaya ambao ulimulika daistopia kwa kina ili kuonyesha makuzi na maendeleo yake. Utafiti huu ulihakiki riwaya teule za Kiswahili *Kufa Kuzikana* (2003), *Dunia Yao* (2006) na *Chozi la Heri* (2014). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kusudi la kuafiki malengo mahsusi ya utafiti huu ambayo ni kuhakiki maudhui daistopia katika riwaya teule za kiswahili; kutathmini mtindo uliotumika katika ujenzi wa daistopia katika riwaya teule na kuhakiki mitazamo ya daistopia katika riwaya hizi teule. Ili kufanikisha utafiti huu tuliongozwa na nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa naye Buffon (1930). Nadharia hii ilikuwa kama dira katika kuzingatia mihimili yake ili kukusanya data mwafaka kukidhi malengo ya utafiti wetu. Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani. Data ilikusanywa na kuwekwa katika makundi matatu makuu yanayoafiki malengo ya utafiti wetu. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu elezi na matokeo ya utafiti yatawasilishwa kwa njia ya kinathari. Matokeo yalikuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya lugha ya Kiswahili kwa kuwa yaliongezea maarifa kuhusu daistopia na jinsi imesawiriwa katika sanaa ya fasihi andishi katika lugha ya Kiswahili.

**Maneno Muhimu:** Utopia, Falsafa, Utandawazi, Kisaikolojia, Teknolojia

**African Journal ofAdvanced Social Sciences**

Volume 1, Issue 1, 2026

## ARTICLE HISTORY

Submitted 21 December 2025

Accepted: 17 January 2026

Published: 26 January 2026

## HOW TO CITE

Syekei, M. N., Nyandiba, C., & Owala, S. (2026). Mitazamo ya Daistopia Katika Riwaya Teule za Kiswahili. *African Journal of Advanced Social Sciences, 2*(1). Retrieved from https://journals.evonexpublishers.com/index.php/ajass/article/view/59

**Published in Nairobi by Evonex Global, an imprint of Evonex Publishers Limited**

© 2026 The Author(s). This is an open Access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution License (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/), which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium, provided the original work is properly cited.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake. Fasihi hugusa na kuacha waja na kuwaathiri ambapo matokeo hupatikana katika maumbo mbalimbali yanayotambuliwa na jamii fulani (Wamitila, 2003). Hii inamaanisha kuwa fasihi ni ufundi ambao hutumia lugha na ina vipengele vitatu vikuu; fani, maudhui, na mitazamo.Vipengele hivi vya fasihi vinasukwa na kufinyangwa na kila mwandishi ili kuuwasilisha ujumbe kwa njia teule. Ufundi huu hubainika wazi kutoka mwandishi mmoja hadi mwingine na huathiri msomaji kwa njia moja au nyingine.

Sanaa ya fasihi imekuwepo na imeendelea kukua tangu karne ya kumi na tisa. Mahsusi, maandishi ya miaka ya elfu moja mia kenda na arobaini na pia miaka ya hamsini yaliakisi ubepari, kisha baadaye yakazuka maandishi yaliyolenga ushosholisti. Katika harakati za kudhibiti jamii za kibepari na kisosholisti, propaganda ilitumika kuendeleza jamii hizo. Lengo kuu la jamii hizo zilikuwa kuonyesha maendeleo ya kijamii na kisiasa. Baadhi ya maelezo ya kitamaduni ya mfumo kamili ya utopia yaliandikwa katika historia ya Marekani katika vipindi kama vile, Zama za Dhahabu mwaka wa 1928 naye Morris Walter, Nineteen Eighty Four mwaka wa 1949 naye George Orwell nacho Woman on The Edge of Time mwaka wa 1976, maandishi yake Marge Piercy. Mikondo ya utopia iliyoakisi masuala mbalimbali ilizuka. Mkondo wa kwanza ulikuwa wa kijamaa uliohusu watumwa na utawala wa kibepari.vMkondo wa pili wa kiteknolojia ulizuka ulioakisi masuala ya maendeleo ya sayansi. Nchi zilibuni vifaa vya kurahisisha mambo kama usafiri, viwanda na mawasiliano. Mwandishi Shaban Robert katika riwaya ya Kusadikika, (1973) na Katama Mkangi katika riwaya ya Walenisi, (2003), ni baadhi tu ya kazi zilizokuwa za utopia au hali shwari. Katika karne ya 19 na 20 neno "utopia" lilibuniwa katika bara la Uropa, katika eneo la Ugiriki ambapo lilimaanisha mahali au jamii bora. Baadaye utopia ilibadilika na kupata mipango isiyo ya kweli na upangaji upya wa mahusiano ya kijamii na kuzuka maendeleo ya sayansi kuhusu jamii, utopia ilipoteza jukumu lake. Upangaji upya wa mahusiano ya kijamii, pamoja na ujio wa utandawazi na athari zake ndipo daistopia ikazuka.

Kulingana na Mukobwa, (1987), wasanii hudhihirisha vipawa vyao kwa namna tofauti tofauti. Waandishi wa kazi za daistopia wana imani kwamba matatizo yanayowakabili wanajamii yanaweza kumulikwa, kukashifiwa na hata kutatuliwa. Waandishi hawa huwa wa kimapinduzi. Huwa na ndoto ya kuwa na jamii mpya inayowahimiza watu katika harakati za kujiendeleza na kujikomboa. Kwa maoni yetu, usomi na kuelezea wanagenzi dhana mpya ni maendeleo katika sekta ya elimu na hivyo basi juhudi za waandishi ni za kushabikiwa na kuenziwa. Hali hapa ikawa isiyo na furaha au kutokuwa na tamaa. Katika harakati zake hizi akazua hali ya utamaushi au udhanaishi. Tutahakiki mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa pamoja na ujio wa teknolojia, elimu na utandawazi tukizingatia athari zilizo wazi za uovu na hasa jinsi zimefanya jamii kubadilika kwa kiwango kikubwa kabisa.

Kipindi cha baada ya miaka ya kati ya 1960 kilitoa riwaya zilizo na sifa mbili kuu. Sifa ya kwanza ikawa ni juhudi kuu ya kutafsiri hasa riwaya za Kiingereza katika Kiswahili. Sehemu kubwa ya riwaya hizo zilijumuika katika mkondo wa fasihi ya Kiswahili. Mtaalamu Kitula, 1999 anasema kuwa riwaya zilizotafsiriwa zimeikwasisha fasihi ya Kiswahili kwa kuiboresha mitazamo na mielekeo yake kwa kuipanua mipaka ya maudhui na maswala yake. Sifa ya pili ilikuwa ni kazi zilizotungwa na zikawa fasihi yenye msimamo wa Kiitikadi. Jamii ilichambuliwa kwa undani zaidi kwa kuhusisha mbinu za kisayansi za uchambuzi. Wakati huu kukazalika riwaya za fasihi ya kisasa. Baadhi ya riwaya za kisasa ndizo zilizobuni kazi zilizotalii dhana ya distopia. Baadhi ya riwaya hizo zilijenga taswira mpya ya kukosoa utopia, kazi hizo ndizo tutazihakiki kubaini dhana ya daistopia. Daistopia ilitabiri mustakabali mbaya kwa wanadamu na kuonya juu ya hatari ya ‘kuwafurahisha watu’. Kipindi kati ya mwaka 2003 hadi 2014 kilisheheni maendeleo makubwa ya kisayansi. Maendeleo haya ya kisayansi nayo yakazua athari katika jamii iliyojaa uozo na uovu. Ni katika ari hii ambapo tutahakiki mitazamo, fani na maudhui katika kila riwaya kama vipengele vya fasihi vitakavyosaidia kumulika suala la kidaistopia. Kazi za hawa waandishi tofauti zimeijenga dhana ya daistopia kwa njia teule.

Utafiti ulihakiki daistopia katika riwaya teule za Kiswahili. Daistopia hujikita katika suala zima la nathari ya kazi za kiubunifu. Kimsingi, daistopia ni mwitikio wa mabadiliko katika jamii. Mwitikio huu huwa kama wasifu wa ndoto ambapo waandishi huzungumzia juu ya nchi ya kidhahania. Waandishi wa kazi za daistopia huonyesha kwamba bado mahusiano ya kijamii hayajakamilika. Katika matini kuna masuala kadha wa kadha ya kumwongoza msomaji katika ulimwengu wa maandishi ya kubuni ikimpitisha katika mpangilio wa matukio, nyakati mbalimbali, simulizi teule, mawasiliano ya wahusika, utendaji na mawazo yao. Haya yote kwa pamoja yanasuka kazi ya kisanii. Hata hivyo kuna mabadiliko katika jamii ambayo hudhoofisha itikadi za kijamii na kuzua mgongano wa harakati rasmi na zisizo rasmi. Shughuli mbili kuu ambazo zinaendelezwa ni udhalimu na ukandamizaji kwa watu. Katika harakati za mabadiliko, kuna kuzuka aina tofauti ya mitazamo, simulizi na mitagusano tofauti baina ya wahusika ambapo daistopia huzuka. Katika usanjari huo, utafiti wetu ulionyesha jinsi waandishi wa kazi teule watatumia lugha kwa ufundi maalum ili ujumbe wao uweze kupokelewa na kueleweka na kuleta athari waliyoidhamiria ya daistopia. Utafiti huu ulionyesha jinsi distopia haijashughulikwa kwa mrengo wa kimtindo. Kwa mantiki hii ndipo tunapata kiini cha utafiti huu ili tulihakiki jinsi daistopia inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.1. Nadharia ya Umitindo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umitindo. Nadharia ya Umitindo imeasisiwa naye Buffon (1930). Kulingana na Buffon mtindo ni ‘mtu mwenyewe’. Hii ina maana kuwa ni ule upekee wa mtu katika matumizi yake ya lugha ili kuwasilisha ujumbe wake.

Mtindo ni dhana yenye utata kuieleza. Msokile (1993) anaifafanua dhana ya mtindo kwa njia mbili. Kwanza, ni namna ambavyo mwandishi ameipa sura kazi yake kifani na kimaudhui na kuitofautisha na nyingine iliyoundwa na mwandishi mwingine. Aidha, anadai kwamba kile kinachoelezwa kinaweza pia kuitwa mtindo. Madai haya yanatiwa nguvu na Ngara (1981), anayeeleza mtindo kuwa ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha; yaani ni jinsi msemaji awasilishavyo ujumbe wake.

Kwa kuchangia dhana ya Umitindo, Crystal na Davy (1969:10) wanasema hivi:

> *Lengo la Umitindo ni kuchanganua tabia za lugha kwa kubainisha sifa mahsusi zilizobanwa katika miktadha maalum kutoka kwa sifa za kijumla za kiisimu ambazo hupatikana katika kila muktadha wa matumizi ya lugha. (TY)*

Miongoni mwa waitifaki muhimu wa nadharia hii ni Coombes (1953), aliyesema kwamba:

> *"Mhakiki ni lazima azingatie vipengele vinavyofanya kazi fulani iwe ya kuvutia. Nia ya mtindo ni kuchunguza na kuchanganua lugha na kaida zake kwa nia ya kutambua mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya kijamii, kufafanua sababu ya vipengele fulani kutumiwa na vingine kuachwa."*

Kwa mujibu wa maelezo haya ni wazi kuwa nadharia ya Umitindo hujishughulisha na namna ya msanii alivyoitumia lugha katika kuwasilisha ujumbe wake. Madai haya yanaungwa mkono na wataalamu wengi katika fasihi wakiwemo (Senkoro, 1982; Wamitila, 2013 na Mosha, 2002). Wataalamu hawa wanakubali kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika mtindo alioutumia mwandishi katika matini husika. Maelezo haya yalitusaidia kuchanganua matumizi ya lugha kidaistopia katika riwaya teule.
Nadharia ya Umitindo huhusisha maelezo ya kiisimu ili kuweza kufafanua dhana zake za kimsingi katika fasihi. Maelezo ya Leech (1969) kuhusu uhusiano uliopo baina ya fasihi na isimu yanaonyesha kuwa dhana hizi zinakamilishana katika utendaji kazi. Anasema hivi:

> *Uhakiki wa mtindo hauhusiani tu na ufasiri wa maana za matini kwa mtazamo wa kiisimu. Nadharia hii kama taaluma haijisimamii pweke bali huhusisha vipengele vya kifasihi na vile vya kiisimu katika uhakiki. Hii ni kwa sababu ya ugumu uliopo katika kuufafanua msamiati mpana wa kimsingi wa kihakiki katika fasihi kama vile sitiari, taswira, kijembe, kinaya, usambamba na jazanda bila kurejelea dhana ya kiisimu. Hivyo basi kwa kuziunganisha taaluma hizi mbili – ya fasihi na ya isimu kiutendaji, nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo inakuwa jukwaa la kushughulikia dhana za fasihi na isimu kwa pamoja. (uk. 2) (TY)*

Kimsingi, Leech anaashiria kuwa uhakiki wa mtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na pia vile vya isimu. 'Hakuna kipengele mojawapo kati ya fasihi na isimu ambacho kinaweza kusimama pweke na kujifafanua kikamilifu'. Hii ni ishara kwamba nadharia ya Umitindo hutumia maelezo ya isimu na fasihi katika kufafanua matini mbalimbali. Hii ina maana kuwa kila tunapohakiki mtindo katika mkabala wa kifasihi hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu pia.

**Mhimili mkuu wa nadharia hii ya Umitindo ni kuchunguza kinachosemwa (ujumbe) na kinavyosemwa (mtindo).**
Mtaalamu Indagasi (1988), anaunga mkono maelezo ya Leech anaposema kuwa nadharia hii hujihusisha na jinsi lugha ilivyotumika kuleta mvuto kisanaa. Mhimili huu ulitufaa katika kuchanganua fani za mwandishi kidaistopia na kuonyesha mbinu za usimulizi zitakavochangia katika riwaya tulizoziteua.
Leech, anaeleza kuwa lengo la nadharia ya Umitindo ni kuchunguza lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengewa kazi fulani ya kijamii. Leech anaonekana kusisitiza kuwa nadharia ya Kimtindo hudhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Fani hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili kusaidia kuwasilisha ujumbe wake. Mhimili huu ulitusaidia kuchanganua lengo la kwanza lililohusisha maudhui ya daistopia katika riwaya teule za Kiswahili.

**Mhimili wa pili, unaelekeza kuwa pana uwiano baina ya ujumbe na lugha katika kazi za kifasihi na vipengele hivi viwili haviwezi kutenganishwa.**
Sintaksia hushughulikia sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi. Sentensi ni kipashio kikubwa zaidi cha kimuundo chenye kuleta maana kamili. Mhimili huu ulitusaidia kuelezea lengo la pili na kiini kikuu hapa kikiwa kuhakiki mtindo jinsi ulivyojenga daistopia katika riwaya teule za Kiswahili.

**Mhimili wa tatu, lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia kuelewa ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi.**
Maoni haya yanaungwa mkono na Tunner (1973), anaposema kuwa uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Matumizi ya lugha huathiri maana. Mhimili huu ulitusaidia kupambanua lengo la tatu ambapo tulipambanua mtazamo wa mwandishi na msomaji kuhusu daistopia katika riwaya teule za Kiswahili.

Mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi yake. Maoni ambayo yanaungwa mkono na Simpson (2004) anayedai kuwa nadharia ya Umitindo husisitiza wazo kuwa kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi. Pamoja na maoni haya, ni yale ya Chapman (1982) anayeelekea kuafikiana na Leech kuhusu jambo hili anapodai kuwa fasihi haiwezi kujadiliwa pasipo kuzingatia kwamba ina matumizi maalum ya lugha. Mhimili huu ulitufaa utafiti wetu kutathmini maudhui kidaistopia katika riwaya teule.

Leech na Short (1981) wameainisha viwango vya kushughulikiwa katika mtazamo wa kifasihi na ambao tutaegemea katika utafiti huu. Hivi ndivyo viwango ambavyo mhakiki anayechukua mkabala wa kifasihi huweza kushughulikia. Kwanza, ni kiwango cha kileksia ambapo aina mbalimbali ya maneno huchunguzwa kama vile nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi na kadhalika. Pili, ni kiwango cha kisarufi ambapo aina za sentensi, uchangamano wa sentensi, aina za virai kama virai nomino, virai vitenzi na kadhalika hushughulikiwa. Tatu, ni kiwango cha kisemantiki ambapo tamathali za usemi kama vile jazanda, chuku, tashbihi na kadhalika hushughulikiwa. Nne, ni mshikamano na mwingiliano wa kimuktadha ambamo dhana za kimtindo huchunguzwa katika mwingiliano wao. Utafiti huu ulihusisha kiwango cha tatu na nne na vilisaidia kuhakiki daistopia kifani na kimaudhui. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na mwanamitindo Leech (1969), mihimili teule ya nadharia hii ilitusaidia kuchunguza daistopia kimtindo pamoja na kuafiki malengo ya utafiti huu.

## Uhakiki Wa Maandishi

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tuliangazia maoni ya waandishi na wataalamu mbalimbali ambao wameshughulikia daistopia. Tutaonyesha namna maandishi haya yanavyohusiana na kutofautiana na utafiti tunaokusudia kuufanya. Katika kurejea mada za kazi hizi, tulizingatia mada zenye vipengele vinavyohusiana na utafiti wetu, hasa kwa kutumia malengo yetu mahsusi ya utafiti.

### 2.1. Asili ya Daistopia

Daistopia imegawanywa katika ulimwengu mbili. Mwanzo ni ulimwengu ambapo maisha 'bora huundwa' na pili ni ulimwengu wote ambapo kila mmoja ana kizuizi cha bandia ambacho hakiwezi kushindwa. 'Dunia bora' ambayo wengi wa wahusika katika daistopia huishi imefanikiwa kwa msaada wa teknolojia na madawa ya kulevya. Nafsi ina uwezo wa kudhoofisha misingi na kuharibu 'ulimwengu bora'. Wahusika wakuu katika huu ulimwengu ni binadamu na jamii yake. Binadamu hapa huchukuliwa kuwa kitu kisichozidi, kisichohitajika na chenye madhara yasiyoendana na jamii yake.

Mollie (2003), daistopia ni mwitikio wa mabadiliko katika jamii hasa mahusiano ya kijamii katika hadithi inayofurahisha. Ni uzao wa safu mpya ya fasihi nzuri ya karne ya ishirini, ambayo ilitolewa kuwakilisha utabiri mbaya wa siku zijazo. Nafasi ya mwanadamu imehujumiwa na ubabe wa serikali dhalimu. Maafa na madhila dhidi ya wanajamii umekolea. Nguvu za kidkteta na woga husheheni jamii hizi na kutawala watawaliwa. Daistopia ni jamii yenye sifa ya kuzingatia kile ambacho ni kinyume na maadili ya mwandishi, kama vile umasikini mkubwa, kutoaminiana kwa umma na tuhuma, serikali ya polisi wakatili na ukandamizaji wa wananchi kwa ujumla. Kila kitu ni kibaya zaidi. Propaganda, woga na udhibiti wa binadamu kwa matumizi ya teknolojia huwa ndizo nguzo zinaoongoza jamii hizi. Maovu ya kijamii huathiri wote lakini wanajamii huyafumbia macho 'ni hali ya maisha' (*Oxford Dictionary,* 1978).

***(Merriam Webster's Collegiate Dictionary, 2010)***, inaeleza kuwa daistopia ni hali au jamii dhahania ambayo wanajamii wanaishi katika hali mbovu zenye hatari kubwa na kwa woga wingi. Tangu enzi ya mwisho ya 'Cold War', waandishi (Bradford, Mallan, Stephens & McCallum, 2003) wanasema kuwa siku zijazo huenda zikawa na majanga makubwa. Majanga haya ni pamoja na utata wa utunzi wa mazingira na athari mbaya zaidi kuwa uharibifu wa mazingira usioweza kurekebishwa.

Mwishoni mwa mwaka wa 1890, *HG Wells, Ray Bradbury* na *George Orwell* wamewapa wahusika wachanga majukumu makuu katika kazi zao zinazodhihirisha daistopia. miaka ya 2000, riwaya nyingi zilibuniwa kwa lengo la kuhifadhi hali mbaya na giza lakini wahusika wakabadilika. Wahusika hapa wakawa sio raia wa kawaida na wasio na nguvu lakini vijana ambao wamewezeshwa, wasio na woga, wenye nguvu na waliodhamiria kutafuta njia za kuishi yenye ushawishi ambayo serikali dhalimu hujaribu kuwadhibiti lakini haziwezi.

Masimulizi ya daistopia hutoa somo kwamba hatua kali za kisiasa zinaweza kuwa jibu halali kwa kutokuwa na haki. Vyombo vya habari na teknolojia huwa na mchango mkubwa katika harakati za uvinjaji wa asasi za kijamii. Hadithi za kidaistopia hutoa picha ya matumizi ya nguvu zaidi kutoka kwa watawala na uwezekano wa ukosefu wa haki na mabadiliko ya hewa hadi uvumbuzi wa kidikteta ulimwenguni. Zaidi, kueneza kwa masimulizi ya distopia kunaweza pia kuhamasisha maoni ya kimawazo. Mchakato wa kihistoria katika distopia umegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni ule utambuzi wa bora. Sehemu hii ni ya awali katika kila asili ya jamii. Sehemu ya pili husheheni majanga, mapinduzi na inajanibisha matukio kwa wakati na nafasi. Sehemu ya tatu, ni baadaye kabisa na hapa wanajamii 'hukubali' na kuishi kwa madhila, ukandamizaji na udikteta.

Kurtz (1970), aligawanya riwaya ya Kiswahili katika kategoria tatu kuu: Mkondo wa kwanza ni riwaya zilizoandikwa pindi tu baada ya uhuru yaani miaka ya 1960. Mkondo wa pili ukawa riwaya zilizoandikwa miaka ya 1980 hadi 2000. Hatimaye mkondo wa tatu ukawa riwaya za ukingo wa 2000 hadi za awali karne mpya. Kwa mujibu wa ugavi huu tuliteua riwaya moja kuakisi mikondo hii ili kuonyesha mabadiliko ya daistopia. Katika harakati za uandishi wa riwaya ya Kiswahili, walizaliwa waandishi kama Said Mohamed, Ken Walibora na Assumpta Matei ambao wameandika kazi zinazoakisi hali halisi ya jamii – daistopia.

Hivyo basi, daistopia ni hali ya waandishi kuonyesha jinsi jamii inavyojaribu kujificha kutoka kwa ukweli wa maisha au ulimwengu wanamoishi. Kuna njama ya kina kuonyesha hali ilivyo mbaya. Kuna mgongano wa mawazo hasa baina ya wahusika ambao huzua migogoro mbalimbali. Migogoro hiyo huzua fujo na ghasia na kuna hali ya 'kujidanganya kuwa hayo ndiyo maisha'.

### 2.1.2. Maandishi ya Fasihi Yaliyolenga Mitazamo ya Waandishi

Mtazamo katika kazi ya fasihi huwa ni mafunzo ya falsafa ya msanii na hubainisha masuala mbalimbali ya kijamii. Mwandishi hufuata au kushikilia jambo fulani kwa imani. Mara nyingine jambo huweza kukataliwa na wengine lakini mwandishi ana uhuru wa kuamua ni lipi la kulishikilia ili kueleza jambo hilo liwe na liwalo. Kigezo hiki huweza kumtofautisha mwandishi mmoja na mwingine. Waandishi wa kazi za kifasihi hujaribu kumulika mambo yanayotukia katika jamii. Katika ile hali ya kuegemea au kuwa na msimamo fulani ndipo kunazuka hali ya mtazamo wa mwandishi au kazi ya fasihi. Ni katika hali hii ambapo tulihakiki riwaya teule kuonyesha jinsi mtazamo wao ni tofauti na wetu. Maandishi yafuatayo yalilenga lengo la kwanza.

Msomi Mutwiri (2005) ametafiti kuhusu utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania na kubainisha mitazamo mbalimbali kuhusiano na nyiso hizo. Mtafiti huyu aliongozwa na nadharia ya Uamali hasa kipengele cha utendi-nenaji. Mitazamo mitatu aliyoiibua ikawa ni ya wanamapokeo, wanamapinduzi na wanamaafikiano. Tofauti na utafiti huu wetu ni kuwa mitazamo tuliyohakiki ni ya daistopia katika riwaya za Kiswahili tukiongozwa na nadharia ya Umitindo

Naye Nyabunga (2005) ametafiti kuhusu "Uhakiki wa *Bina-Adamu*! (2002) na *Musa Leo! (2004)* za K.W. Wamitila" katika misingi ya Nadharia ya Uhalisiajabu. Katika utafiti wake, Nyabunga anachunguza kwa undani suala la uhalisiajabu katika riwaya hizi mbili za kimajaribio kwa kuongozwa na mihimili kadhaa. Utafiti wetu ni tofauti kwa kuwa ulijiegemeza riwaya tatu za waandishi tofauti na ulilenga kuhakiki mtazamo wa daistopia tukiongozwa na nadharia ya Umitindo.

Msomi Odhiambo (2004) alihakiki misimamo iliyochukuliwa na waandishi wa fasihi pendwa wa miaka ya 1970 na 1980 kama mwendazake Chris Wanjala, Elizabeth Knight na Bernth Lindfors. Anaeleza kuwa kuna haja ya kutenga fasihi pendwa na yenye mashiko katika lugha ya Kiingereza. Mtafiti huyu aliongozw na nadharia ya Fasihi Linganishi. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tulizamia riwaya za Kiswahili na tukiongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Pia kipindi chetu ni tofauti kwa sababu tulianzia miaka ya 2003 hadi 2014, miaka iliyoafiki riwaya teule.

Naye Mbugua wa Mungai (2007), alitafitia diskosi ya magari ya usafiri almaarufu 'Matatu'. Aliangazia kikundi ja jamii kilichojaa fujo na lugha teule. Alionyesha jinsi sekta hiyo ya usafiri inajihusisha na uovu kwa sababu ya kutengwa. Utafiti wake ulilenga wahusika wa kiume tu kwa kuongozwa na nadharia ya Usasa. Data ya utafiti wake aliitoa nyanjani. Utafiti wetu uliangazia maisha ya wananchi wote kwa ujumla na changamoto katika asasi zote kwa mtazamo wa kidaistopia. Nadharia iliyofaa utafiti wetu ni ya Umitindo. Data nyingi iliyotufaa tuliidurusu maktabani na riwaya teule za Kiswahili.

Khainga O' Okwemba (2009), katika ushairi anaeleza hali ya dharura kwa kuonyesha harakati za wahusika kupigania haki. Mtafiti huyu alizamia kipera ya fasihi andishi cha ushairi wa lugha ya Kiingereza uliondikwa na Philo Ikonya na aliongozwa na nadharia ya Ulimbwende. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tuliangazia mtazamo wa waandishi wa riwaya za Kiswahili na tukiongozwa na nadharia ya Umitindo. Hata hivyo, utafiti huu ulinufaika na ufumbaji uliotumika na mshairi huyu kumulika daistopia kutoka simulizi za riwaya.

Kahinde (2010), alitathmini vizuizi katika umma ya taifa la Nigeria jinsi waandishi wa riwaya za Kiingereza walivyosawiri. Riwaya zilizomfaa zilikuwa *Anthills of the Savannah* ( Chinua Achebe, 1987), *The Famished Road* (Ben Okri, 1991), na *Purple Hibiscus* (Chimamanda Ngozi Adichie, 2003). Nadharia iliomwongoza ni ya Uamilifu. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tulilenga kuonyesha mtazamo wa waandishi teule katika kufafanua dhana ya daistopia tukiongozwa na nadharia ya Umitindo katika riwaya teule za Kiswahili. Pia riwaya zetu ni za kulenga mataifa mbalimbali dhahania na sio taifa moja.

Bakari (2011) ametafiti kuhusu usemezano katika mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka, Bina-Adamu* na hadithi fupi *Sadiki Ukipenda*. Amejadili historia fupi ya uandishi wa waandishi Said A. Mohamed na K. W. Wamitila na kuonyesha jinsi walivyobadilisha mtindo wa uandishi kutoka uhalisia hadi uhalisia ajabu. Utafiti wake unadhihirisha jinsi uandishi wao na umuhimu wa kufanya hivyo ili kuonyesha hoja zao kwa uwazi zaidi katika hali zinazobadilikabadilika. Utafiti huu ulitufaa kwa kutuelekeza kutambua mitazamo ya waandishi jinsi unavyoibua mtazamo fulani. Waandishi wa riwaya teule za utafiti huu wameibua mitazamo wa daistopia ambayo tulihakiki na kuweka matokeo wazi na kwa kina kinachosheheni ongezeko la maarifa. Tofauti zaidi zinazuka katika nadharia ambapo mtaalamu huyu aliongozwa na nadharia ya Usemezano nasi tuliongozwa na nadharia ya Umitindo.

Chepkwony (2012), katika makala anaeleza kwamba machafuko ya eneo la Molo yalibuniwa ili kuafiki mtazamo fulani kuhusu siasa za taifa la Kenya. Mwisho wa haya machafuko yalikuwa vifo na ghasia iliyosababisha hasara kubwa kabisa. Mtafiti huyu aliongozwa na nadharia ya Historia Mpya. Sawia na utafiti wetu ni kuwa tulionyesha jinsi historia na fasihi ni vitu viwili vilio na ukuruba mkubwa. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tuliangazia riwaya ya Kiswahili tukiongozwa na nadharia ya Umitindo. Mtazamo wetu ulimulika daistopia iliyoendelezwa na waandishi katika fasihi.

Mutua (2017) alichunguza mitazamo ya waandishi wa kike na kiume kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Waandishi waliwapa wahusika sifa mbili kuu aidha chanya au hasi. Mtafiti huyu aliongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Baada – Ukoloni. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa tulihakiki mitazamo ya waandishi kuhusu daistopia katika riwaya za Kiswahili tukiongozwa na nadharia ya Umitindo.

### 3.0 Mitazamo Ya Daistopia Ilivyowasilishwa Katika Riwaya Teule Za Kiswahili

Mwandishi wa kazi za fasihi hulenga kuweka wazi mafunzo ya hali halisi kisanaa. Katika harakati za kuweka mawazo na mafunzo katika kazi za fasihi, mwandishi, mtunzi au msanii wa kazi za sanaa hugundua kuwa pana falsafa ambazo alikusudia ziwafikie wapokeaji wa kazi zake. Zinaweza kuwa falsafa nyingi au hata moja. Hii ina maana kuwa pana mchujo wa welekeo wa mawazo muhimu yajitokezayo kila mara katika kazi za fasihi. Wakati mwingine waandishi zaidi ya wawili wanaweza andika kazi za fasihi zinazolingana na kuingiliana kimtazamo au kifalsafa. Wasanii hawa wanazungumzia mambo yanayoathiri jamii wanaliyozaliwa au walimolelewa.

Katika fasihi ya daistopia waandishi wametumia kazi za uandishi kama kioo cha kuangalia changamoto au hatari zinazokabili jamii ya sasa. Mitazamo hii ilitoa njia tofauti za kuangalia na kufasiri daistopia zikileta mwelekeo tofauti juu ya maana, ujumbe na onyo. Kazi za fasihi zilisheheni ujumbe wa mkondo fulani wa filosofia. Waandishi hutumia wahusika kuweka wazi mitazamo yao. Ifuatayo ni mitazamo mbalimbali inayotumika kuelewa na kufasiri daistopia.

Hali mbaya katika maisha ya jamii mara nyingi hugusa masuala ya kitabaka na maadili na kuzalika hali nyingi tatanishi. Maingiliano ya viumbe vya kigeni na mitagusano na teknolojia huzua vipengele vya kijamii vya itikadi za kisiasa vinavyoshangaza. Athari ya haya ni vita au fujo baina ya binadamu na mawazo yao, jamii yao, na ulimwengu kwa ujumla.

### 3.1 Mtazamo wa Kisiasa

Serikali au viongozi wanaendesha utawala wa kidikteta. Raia wanaosawiriwa huwa ni wale waliokosa uhuru wa kujieleza au kuchagua viongozi wao na wanaolazimishwa kufuata sheria kali ambazo zinazuia uhuru wa kujieleza, kushiriki katika maamuzi au hata kufurahia haki zao za kimsingi. Mfumo huu ulilenga kukandamiza fikra za watu na huathiri binadamu vibaya. Kimsingi wanajamii walikandamizwa kisiasa, walidhibitiwa na serikali na walinyanyaswa na madaraka.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatudondolea mjadala uliokuwepo kati ya Tila na baba yake Ridhaa. Mjadala huu unatokea katika kumbukizi tu baada ya Tila na wengine kuangamia katika mkasa wa moto. Siasa ndicho kigezo kikuu katika ukuaji wa kiuchumi katika mataifa mengi ya duniani. Ukuruba kati ya uchumi na siasa huwezi sambaratishwa. Mwandishi anasema:

> Tila: Mwalimu Meli alitueleza jinsi mifumo ya uzalishaji mali ilivyobadilika, kuanzia wakati wa ujima, ikabaila, ubwanyenye, ujamaa hadi sasa tunapopambana na utandawazi.
>
> Tila: ... upo uhusiano kati ya mfumo wa kiuchumi na mfumo wa kisiasa. mifumo hii miwili hudhibitiana. Utawala huteuliwa maksudi kuendeleza mfumo uliopo wa kiuchumi kwa maslahi ya watawala na tabaka ambalo linazimiliki nyenzo za uzalishaji mali. (uk. 38-39)

### 3.1.2. Mtazamo wa Kimaadili

Jamii hushuka kimaadili. Maadili yamepotea na uovu umeenea. Misingi ya haki, utu na huruma hufa. Maovu kama ufisadi, maafa na unafiki hukolea. Hutumika kukosoa mifumo ya kisiasa au kijamii ya kisasa. Inachambua udhibiti wa serikali, ukandamizaji wa watu au usawa wa kijamii. Mfumo huathiri utu na tabia ya binadamu.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida anapofika jijini, kesho yake alitoka mapema kwenda kununua gazeti ili apate habari za kwao Baraki. Alisaka hadi akapata na katika harakati hizo akapotea njia na kuamua kupumzika katika bustani moja. Katika ile bustani ndipo alisikia mwanamume mmoja akimweleza mwenzake aliyeitwa Ninja sifa za vigoli waliokuwa wakikoga maji ya mtaro pale bustani. “Usivione vidogo hivyo,” ...”Manze usiku vinakwenda na watu wa Mapajero na Mabenz. Wanaume wazima wenye nafasi na uluwa za hali.” (uk. 33). Hii hapa ni kuonyesha upotovu wa maadili katika jamii. Akida alipatwa na usingizi na alipoamka akapata viatu vyake vimeibwa akawashuku Ninja na mwenzake kwa sababu walikuwa wametoweka. Akida anatueleza:

*Usingizi ukanijongelea asteaste nikalala unono. Nilipozinduka ilikuwa nadhani saa saba hivi. Nilitazama alipokuwa Ninja na mwenzake. Patupu. Nikahisi kiupepo baridi kinazipiga nyayo za miguu yangu. Kuangalia vizuri, nikaona sina viatu. Vimeibwa! ...Bustani hakuliki tena. (uk. 33).*

Akida anapodhalilishwa na sekretari kwa kuitwa 'chokora' anakumbuka aliyomuasa baba mzazi. Kila wakati baba alimsihi kuacha hasira maana huenda akazua hasara. Anatusimulia:

Nasaha ya baba dhidi ya udhaifu wangu ikanijia dhahiri shahiri. "Akida hasira yako itakuja kukuzulia baa mawnangu usipoidhibiti," baba alikuwa heshi kunishauri. Ubeti wa utungo wake mwenyewe alionikaririsha kila uchao nyumbani ukanifyatuka akilini:

Hasira hasara, mwanangu nayo usiwe

Epuka harara, hata vipi utusiwe

Simama imara, jidhibiti usifiwe (uk. 42)

Mwandishi anatusimulia kuwa hata kumwona Waziri wa Elimu sio rahisi. Pam na Akida walienda katika Ofisi ya Waziri wa Elimu nusura wafukuzwe. Utaratibu wa mambo nikuwa lazima awe amekualika. Akida anatusimulia:

Nilipoingia ofisini na Pam, sekretari alituuliza kama tulikuwa tuna miadi na waziri. Kumbe huwezi kumwona waziri bila kufanya miadi? (uk. 47). Hili ni dhihirisho wazi kuwa ofisi za umma sio mahali pa kuzurura ovyo. Maadili na utaratibu unafuatwa. Akida alipojitambulisha na kumtolea sekretari hati ya matokeo ndipo aliporuhusiwa kujiunga na wenzake pambajioni.

Kasisi John aliwahubiria akina Tim na Akida kuwa tufuate maadili mema huku akihimiza, akielekeza, akiamuru, alionya na hata kutoa vitisho vitakatifu. Alihuburi:

*"Maandiko yanasema waasherati hawatarithi ufalme wa Mungu;" ..."Vifisheni viungo vyenu vilivyoko duniani kuhusiana na zinaa. Usingoje mpaka ubebe ukimwi ubakie kilo mbili ndipo uje kwangu unalia 'Eeh! Kasisi niombee!" ..."Ndugu na dada mmepotea mkawa kama watu wa ulimwenguni," ..."kwa nini mnaruhusu ukabila kuingia kanisani. Kisa cha kumkataa mhubiri James Sanya kwa sababu ya ukabila kimetia doa kanisa. Eeh! Fikiria askari kuja kanisani kuzima ghasia niongoni mwa waumini! ...Tuna tofauti gani na makanisa Wilayani Korosho yaliyoshindwa kupatanisha watu yakawaacha wakauana burebure?..."(uk.121)*

Jerumani anamwambia Akida kuwa aibu kubwa ni maovu ya ukabila bali sio makabila yetu. Anaonya kuwa tunapaswa kutumia dini kutugeuza mioyo, bali si dini kutumiwa kama mahali pa kujificha na kuwaangamiza wengine. Dini ndicho chombo cha kuhubiri maadili bali sio kuporomosha maadili. Jerumani anaeleza:

*"Dini? Wewe unaishi dunia gani Herr Madodo Kipande? Hujasikia Makasisi Wakorosho walivyowaua waumini wenzao? Wakanju waliokimbilia usalama makanisani huko Korosho? Hujasikia nyumba za makasisi ndizo zilizokuwa mabohari ya bunduki, nyuta na mishale ya kuwamaliza watu Korosho? Mambo yaleyale yaliyokuwa Rwanda na wanadini kusahau dini na kuwaua wanadini wenzao kwa sababu ya kikabila. Hujasikia mizozo na migawanyiko makanisani, mahekaluni na misikitini? (uk. 156)*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Kilua, mwanawe Ndi- anakigawa chakula chake na kukitega pembeni kwenye kizingiti cha mlango kuingilia chumba cha baba yake. Baba yake alipotoka msalani haja ndogo, alikipata pale. Kero ya njaa na barua vikamshawishi kuvichukua. Barua ilieleza kuwa chakula ni cha halali na bali si cha ukahaba, *...Si chakula cha ukahaba* (uk. 57), wa Bi. M na mgao alioupata ni nusu ya mgao wake Kilua. Ndi-alikuwa ameghairi nia afe njaa badala ya kula chakula cha ukahaba. Sasa alibadilisha mawazo na kuhalalisha maana hata mgao ulikuwa mdogo lakini ulikuja kwa wakati ufaao, wiki nzima hajala chakula vizuri.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatuelezea mabadiliko ya nyenzo za kuhusisha ili usalama udumishwe ndiposa maadili yawepo. Haya yaliwekwa wazi katika hotuba ya Apondi, ambapo Mwangeka ni mmoja wa waliohudhuria kongamano hilo. Hii ni kumbukizi aliyokuwa nayo Mwangeka anapojaribu kutusimulia jinsi alivyotekwa na sauti yake Apondi akihutubu. Baadaye Mwangeka alijasiria na kuweza kumposa na kumuoa Apondi. Apondi anahutubu:

*"Suala la polisi na wanajeshi kutatua mizozo midogomidogo kwa makeke na bunduki ni jambo ambalo limeanza kupitwa na wakati; ni sawa na kumuua chawa kwa fimbo! Raia wanahitaji zaidi ushauri badala ya vipigo. Kutatua tofauti zetu kwa vita ni kama kufukuta moto zaida, na amani tuliyoazimia kupata haipatikani. Vilio vya raia kuhusu kile wana-*

*chokiita extra judicial killings vimehanikiza kote. Huenda tusiwe wahusika katika visa hivi. Hata hivyo, ni vyema kutahadhari kabla ya hatari. Wakati mwingine, ndugu zangu, amani haiji kwa ncha ya upanga!"...'Ulingo wa Kwae haulindi Manda.' Jukumu la kudumisha amani na usalama ni letu. Usalama hauji bila ya kujitolea mhanga. Na kujitolea mhanga huku si kushika bunduki tu, bali pia kujiasa dhidi ya njama za kifisadi na nyendo nyingine hasi. (uk. 113)*

Mwandishi anatusimulia kuwa baada ya mtandao wa Sauna na Bi. Kangara kutibuliwa, polisi waliweza kutiwa mbaroni na kuwafikisha mahakamani ambapo walishtakiwa kwa kosa la ukiukaji wa haki za watoto, wakarambishwa miaka kadhaa gerezani na kazi ngumu (uk. 158).

Mwandishi anatusimulia jinsi Dick alivyofaulu kwa kubadilisha mienendo kisa na maana hapo awali alikuwa anajihusisha na kulangua dawa za kulevya. 'Nimekuwa kielelezo kwa vijana wengi ambao awali waliamini kwamba mhalifu hawezi kubadilika na kuudhibiti mustakabali wa maisha yake. Yote haya yamewezekana kutokana na mwongozo mlionipa nyinyi.' (uk. 174).

### 3.2. Mtazamo wa Kijamii

Jamii inaonyeshwa kuwa imegawanyika vibaya kati ya matajiri na maskini, huku wale walio madarakani wakiwa na uwezo wa kudhibiti raslimali zote. Maskini au watu walio wa hali ya chini wanakandamizwa na kushindwa kupata mahitaji ya kimsingi huku watu wenye mali wakiishi maisha ya anasa. Hali hii inasababisha ukosefu wa haki, usawa na matumaini miongoni mwa raia wa kawaida. Mfumo mbaya wa kijamii huchafua utu na huzua ukosefu wa usawa wa binadamu. Familia, elimu na afya ni asasi tatu kuu za kuendeleza jamii.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida alimthamini sana Tim hasa kumpa makazi na usuhuba wao kudumu hadi kifo ingawa walitoka katika jamii tofauti. Akida anawasiliana na Tim kupitia barua na alimwamini kuwa angemchukua pale kituo cha basi Tandika. Anamwita shemeji ilhali hana dada ambaye Tim angemwoa kwa kuwa alikuwa mtoto wa kipekee kwao. Tim alikuwa na dada aliyeitwa Tamari lakini Tamari alimdharau Akida. Urafiki kati ya Akida na Tim ni wa kufuata kunga za kijamii na kukiuka uhasama wa kiukoo. Akida anatueleza:

*Tamari aliniona kama mkia wa mbuzi, kuzaliwa kwangu hasara kwa dunia. Kutaraji kumwoa Tamari kulikuwa kutegemea jambo muhali kabisa, kama kutafuta meno ya kuku. Aidha Tim hakuwa na mtu wa kumwoa kwetu; mimi sikujaliwa kuwa na dada. Isitoshe ndoa baina ya kabila langu na la Tim hutokea kwa nadra sana. Makabila yetu yana uhasama wa jadi kila moja likijifutua na kubeua jingine. (uk. 8)*

Baada ya vita kuzuka Baraki, Tim na Akida wamewawatafuta wazee wao hospitalini na mochware bila mafanikio. Jioni moja baada ya kutoka Hospitali ya Rufaa ya Tandika bila mafanikio, Tim anamtembelea Tom, mwanawe Mzee Mangala. Tom alikuwa amefanikiwa kusomea Maarekani na kumwoa Mzungu. Mwandishi anatuelezea mtazamo wa jamii kuhusu kusomea ng'ambo na kazi duni waliosalia kusomea kijijini. Wazee wa Baraki walipenda kusema;

*"Majuzi tu nimemwona mtoto wa Mangala bado mkembe anaramba kamasi. Sasa amekuwa msomi hasa na tena kumwoa Mzungu."*

*"Nikidhani pengine atakuwa fundi wa viatu au hamali."*

*"Ya Mungu ni mengi yakha."*

*"Tuseme mtoto wa Mangala ana bahati nzuri,wajua siku hizi hata wasomi huwa utingo na matopasi." (uk. 80)*

Akida na Tim wanapomtembelea Tom, mwanawe Mangala kumjulia hali na wapashane habari zaidi kutoka kijijini, wanampata mkewe Mzungu aliyewakaribisha na kuwapa vinywaji. Huyu mke Mzungu anashangaa kwa nini baba mkwe kakataa kuishi nao ilhali ni mjane. Hata kutaja jina la baba mkwe ni kuvunja mwiko. Na wanatueleza zaidi kuwa hata akifa, Mzungu ataruhusiwa kwenda matangani baada ya yeye kuzikwa (uk. 83). Haya ni masuala ya kijamii yanayoshilikiwa kwa miaka na mikaka hata kama Tom amesomea ng'ambo na kuona mengi.

Matanga ya Mzee Mangala lazima yafanywe kwake Baraki. Hii ni kwa mujibu wa mila na desturi. Tom anasema: "Babangu si mbwa koko, alikuwa mtu na kwake ati. ...Tim kitembo cha elimu ya mtu hakihusiani hata chembe na itikadi zake. Mimi naamini mwacha mila ni mtumwa. Pengine hiyo dini yako ndiyo inayokupa kufikiri hivyo (uk 91). Kwa mujibu wa Tim, usasa angemzika Tom angemzika baba yake makaburi ya umma Jijini Tandika.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Ndi- antueleza jinsi kompyuta ilikuwa mwokozi wake katika maisha ya upweke na unyamavu. Sasa nitakuwa na mwenzangu zaidi wa kusema naye. Ilhali anaogopa kuwa dunia itamwona kwa lensi tofauti. Sijawahi katika maisha yangu kutaka kukanyaga na kusagasaga watu wa nguvu za kipawa changu. ...Wala sijawahi kuota kuwa na ukwasi na ujeuri, kiburi na kuvimbisha kichwa (uk. 8).

Mwandishi anatwambia kuwa Mzee Uledi alifanikiwa kuoa na akamwoa Biti Jabu. Hawa wawili wakafanikiwa na watoto lakini hulka yao ya ulevi ikawapa raha maishani mwao. Jamii ikawakumbatia jinsi walivyo walipokosa kubadilika. Ndi- anatusimulia:

> *Biti Jabu aligeuka na kuwa mfuasi wake, akawa mlevi mwenziwe. Wakazaa watoto lakini watoto hawakuwa sababu ya kuwaondoshea raha zao. Mtaa mzima ulimchukia kwa ulevi uliomzidi. Lakini mwishowe mtaa uliwazoea wote wawili kwa ulevi wao. Hawakujali mtu yeyote na watu hawakuwajali wao tena. (uk. 39)*

Ndi- yu mwingi wa uchungu kuhusu mkondo ambao bintiye ameuchukua. Anashuku huenda jamii ikatoa hukumu yake lakini kwa kiwango kikuu familia ndiyo itapata lawama. Ndi- anatueleza:

> *Mimi nimeathirika pande mbili katika jambo hili. Kwanza, ni babako. Lazima nione uchungu. Na pili, najua vizuri kwamba kuna wahalifu wakubwa zaidi kuliko wewe. Wao ndio wa kulaumiwa. Wameharibu kila kitu chetu. Maisha yetu sote. Ya sisi na nyinyi vizazi vyetu, vya leo na vijavyo. (uk 108).*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatueleza jinsi enzi za zamani, jamii ziliishi kwa pamoja na amani. Ardhi ilikuwa yao kwa jumla. Kabla kuwasili kwa wakoloni, umiliki wa ardhi ya kibinafsi haukusisitizwa katika jamii zao. Watu waliishi na hata kulima mashamba ya majirani, marafiki na jamaa. Mashamba hayakununuliwa. Ridhaa anasimulia:

> *Mkoloni alipofika, alipuuza sera za Mwafrika za umiliki wa ardhi na kuamua kujumuisha pamoja ardhi iliyomilikiwa na mtu binafsi, na kuidhinisha umiliki wa hatimiliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii. Katika sera za kijadi ya umiliki na matumizi ya ardhi, raia wote, hata wageni, walikaribishwa na kugawiwa mashamba, hivyo kupata mbinu za kuyaendesha maisha. (uk. 10).*

Hatimiliki na pesa vilisababisha mshikamano wa kijamii kuvurugika. Sera mpya ya umilikaji nafsi wa ardhi ilimaanisha kwamba wale waliokosa pesa za kununulia mashamba wangekosa mahali pa kuishi. Na hata waliobahatika kuwa na pesa za kununulia mashamba daima walichukuliwa kama wageni wasiopasa kuaminiwa.

Ridhaa na wenzake walirudishwa nyumbani kwao kufuatia mradi ulioitwa na wanaharakati wa kupigania haki za kibinadamu: *Operesheni Rudi Edeni.* Pale Msitu wa Mamba alikutana na akina Selume na kujenga udugu mpya katika mazingira ya uhamisho. Ridhaa anatueleza jinsi hali hii yake mpya ilivyompa mtazamo tofauti wa kijamii. Udugu na utangamano na wakimbizi wenzake uliyahuisha maisha yake, ikayajenga upya, ukamfunza zaidi kuhusu thamani ya binadamu. (uk. 35).

Mwandishi anatusimulia jinsi Bwana Kiriri alivyowarai wanawe warejee nchini kwao baada ya kuhitimu kusomea ughaibuni. Hawakurejea na Bwana Kiriri akabakia kuanza kukubali watumishi wake kama jamaa zake, ndivyo Kangata na mkewe wakaja kuishi kwao kwa muda mrefu baada ya Kiriri mwenyewe kufa. Mwandishi anasema:

> *Bwana Kiriri aliachiwa watumishi na vimada wake, kama alivyodai mke wake, Annette. Baada ya wana wa Kiriri kumaliza masomo yao, walibakia huko huko Uzunguni kufanya kazi. Baba mtu kila mara akiwarai kurudi nyumbani angaa kusaidia kuziendesha baadhi ya biashara zake lakini kila mmoja alishika hamsini zake huko ng'ambo. "This country has nothing to offer. Nchi ambayo hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mishahara ya mkia wa mbuzi! Mimi sitakufa maskini. Acha niwekeze huku mbali ambako sina hofu ya mali yangu kuibwa au kuchomwa na waivu wangu," alisikika akisema Songoa, kifunguamimba wa Kiriri. (uk. 65).*

Mwandishi anatusimulia zaidi kuwa baada ya Sauna na Bi. Kangara kukamatwa, Mwaliko ambaye alikuwa bado chini ya malezi ya Sauna ajenge mbavu kabla kuuzwa, alihojiwa na polisi ajaribu kukumbuka kwao hata wazazi wake. Lakini hakuweza kwa sababu walikuwa wamelanguliwa wakiwa wadogo. Polisi walimpeleka Mwaliko katika kituo kimoja cha watoto mayatima kilichoitwa *Benefactor* (uk. 159). Kituo hiki kikawa kama nyumbani na jamii kwa Mwaliko ambapo aliweza kuendelea na masomo yake.

Mwandishi anatuelezea mtazamo wa kijamii uliomridhisha na kumnufaisha Dick. Mwaliko na Dick wamelelewa na Mwangeka na Neema, 'Mlinipokea kwenu japo hatukuhusiana kwa damu wala usaha' ...Zaidi, utulivunilioupata nilipoambulia familia hii ulinipa msukumo kila mara nilipokabiliwa na ndaro. (uk. 174). Dick anawashukuru wazazi hawa walezi waliojawa na heshima na upendo.

### 3.2.1 Mtazamo wa Kisaikolojia

Huchunguza saikolojia ya binadamu chini ya hali mbaya. Wahusika wanajinasua vipi au wanaathirika vipi kisaikolojia kutokana na mazingira ya ukandamizaji.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, kifo cha mwalimu Alex kinaonekana kuwa mwisho wa matatizo ya akili yaliyomsibu. Hata hivyo mambo kama kupayuka ovyo, kusema na vichaka na kusalimu ng'ombe yalisemwa naye Akida kuwa aibu kwa msomi wa Historia na mwalimu aliyebobea katika taaluma yake. Kifo kinaonekana kuwa kitampumzisha Mwalimu Alex kutokana na changamoto za kisasaikolojia zilizokuwa zimemwandama. Akida anatwambia:

> *Katika siku zake za mwisho Mwalimu Alex alikuwa mwehu. Labda kifo kilikuwa aula. Labda jamaa zake wangeondokana na fedheha. Wapo wanaosema, mwendawazimu anapotembea uchi, wanaofedheheka ni jamaa zake. (uk. 5)*

Akida anatukanwa na sekretari katika ofisi ya Bwana Gembo, "Na we '*chokora'* unataka nini? (uk. 41). Akilini mwa Akida hasira zikampanda. Akida anatueleza:

> *Hisia za aibu iliyeyuka, akanipanda Ibilsi wangu:hasira. Laiti mwanamke huyu angalijua anacheza na cheche za moto, utamwunguza. Nilitaka kumparamia nimchanechane, nimpondeponde, nimsagesage, nimsongoesongoe. Si amwulize Mariamu aliyenitukana shuleni 'asojua wanakotahiriwa' nikamzaba konde akazirai? Kama si kufanyiwa msaada wa kwanza angalikuwa marehemu. ...Si amwulize Matata aliyenitukania hayati mamangu karibu nimtoe jicho? (uk. 41-42)*

Akida yumo katika ruja ya mawazo kuhusu yaliyokuwa yakitendeka kwao kijijini Baraki. Hata baada ya mazuri kumtendekea kama kusalimia Waziri, kuzawadiwa na kitabu cha baba kuchapishwa, anajiuliza maswali mengi yasiyo majibu. Anajizungumzia mwenyewe:

> *...Nimo katika kijumba cha Tim. Nimetingwa na mawazo tele. Jana tu nimemwona waziri, nikamsalimia mkononi, akanipa zawadi. Sasa simfikirii. Jana tu zawadi yangu, nisiyopata kuijua ilikuwa nini, imepotelea garini. Lakini sasa siifikiri. Jana jioni nimelimbuka kujiona kwenye kioja kiitwacho runinga nikipokea zawadi kutoka kwa waziri. Lakini linifikirishe nini hilo? Jana tu nimeshuhudia ufanifu wa babangu katika fani ya uandishi; sikuona tu, nilipewa nakala za kitabu chake kilichochapishwa kumpelekea. Ila sasa fahari hiyo naiona ombwe tupu. Tim karauka mapema...Sijalala usingizi, nimejilaza tu kitandani. (uk. 58).*

Akida na Tim wanaomboleza kuhusu habari ambazo Tom alikuwa amewapa kuhusu Baraki. Anamwelezea Akida kuhusu chanzo cha vita. "Usiulize wanapata wapi silaha..."Muhimu hapo ni chuki. Chuki hushinda bunduki ati. Wakorosho na Wakanju wanauana kwa sababu za chuki ilhali wameishi eneo moja kwa muda mrefu. Matatizo yao yanazuka kutoka imani na athari za kisaikolojia.

Tamari anapoendelea kupata nafuu kwake nduguye Tim, anakumbuka aliyoyashuhudia kule Baraki na hili linamsababbishia kupiga unyende nusura ampasue Akida viwambo vya masikio. Tim anlimuuliza: "Nini?" Tim alisaili. "Nimemwona mwuaji," alisema na kumwashiria Akida. "Anataka kuniua!" (uk. 87). Hii ni ishara wazi kuwa vita vile vilighafili Tamari kisaikolojia na yeyote Mkanju kwake ni muuaji.

Tom, Tim na Akida walizuru Nyumba ya maiti wilayani na kweli kuthibitisha kuwa mwili wa Mzee Mangala uko pale anakubaliana naye kuwa vita hivi vya kikabila havikufaa kuwepo. Tim anasema: "Basi muhimu watu wabadilike akilini na moyoni. Mtu ajue wewe ni kabila gani, ila asikuchukie kwa msingi wa kabila lako (uk. 90). Hapa anazua mtazamo wa kisaikolojia kuwa ni vyema mtu kujidadisi akilini na kufanya uamuzi wa kumpenda kila mtu bila kubaguana na misingi ya kikabila.

Mwandishi anatuelezea zaidi safari ya Tom kumzika Mzee Mangala. Walipopita Mto Kibisi Akida anakumbuka jinsi walivyopiga mbizi pale akiwa mdogo na wenzake walipowaleta ng'ombe kunywa maji. Katika kumbukizi zake anatudondolea mawazo mengi yanayoiteka akili yake:

> *Maji ya Mto Kibisi yalinyiririka kama nyoka chini ya kidaraja. ...Yalijiendea shwari, hayana habari kwamba Baraki kumetumbukia nyongo. ... Hauna habari juu ya roho zilizoteketea kwenye vita vya kikabila ng'ambo zake zote mbili. Nilitazama jinsi mo huo unavyojipitia salama usalimini, kama ulivyofanya tangu kale na ule, nakatamani wanadamu waaminike, iwafafanukie kuwa vita havina macho (uk. 95).*

Akida amefaulu kuuchomoa mshale uliokuwa kifuani mwa Tom. Kwa bahati nzuri akapata toroli aliyoitumia kumsukuma Tom hadi barabara kuu kuelekea Tandika usiku. Alijasiria kusimamisha *Land Rover* moja ambalo waliokuwemo ni mwanamke na mwanamume waliokuwa wakifanya kazi ya shirika la kutoa msaada la *Action Men*. Wasamaria hawa wema wanasaidia Akida kumweka Tom na kufululiza hadi hospitalini Korosho. Akida aliketi nyuma ya gari hilo. Akilini mwa Akida alizama katika ziwa la tafakuri:

> *Fikira juu ya hayati mamangu na upendo, uanana, na ucheshi wake zilinipitikia akilini. Fikira juu ya babangu niliyemwacha mgonjwa na sasa sijui hali yake, zilinisumbua akilini. Fikira juu ya Tom aliyefumwa mshale kifuani si wa maji si wa chakula...Akifa basi ndoto yangu kwenda Ughaibuni haitatimia. (uk. 109)*

Jerumani anamshauri Madodo Kipande almaarufu Akida kuhusu kuondoa aibu na kufanya kazi. Hii ni baada ya Akida kumdhalilisha kuwa yeye aliyekuwa mwanafunzi Ujerumani lakini sasa anakokota rukwama na kuwatekea watu maji. Jerumani anasema:

> *"Aibu ya nini? Mimi si bwana mkubwa wa watu hao wa Sangura. Mimi ni mtumishi ati. Nimeona Ujerumani matopasi na wafagizi wakizifanya kazi zao kwa kujituma. Ndiyo maana tunapaswa kufumua mioyo yetu na kuifuma upya. Hiyo ndiyo siri ya maendeleo..." (uk 156)*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mhusika Ndi- anaaamua kujitenga na familia yake na kuwana mwandani wake ambaye ni kompyuta huku kajifungia nyumbani kwake. Hapa ni kuwa na mawazo na kubadili uhusiano wa watu na vifaa:

Wengine wote watoto wangu wapo hapahapa, lakini nimewapoteza. Au, bora niseme wamenipoteza. Au, tumepoteana hapo lakini mbele ya macho yangu na mimi mbele ya macho yao. (uk. 6)

Mwandishi anatuelezea zaidi kutokana na mazungumzo baina ya Ndi- na nafsi yake kuwa, dunia imetawaliwa na imedhibitiwa na wenye pesa na mali. Anaposema:

> *Wenye nguvu za utawala, si wenye akili tena, ni wenye mali na pesa na nguvu za kijeshi. Hao ndio wanaohodhi utaratibu wa maisha, nyenzo za mawasiliano, elimu, sayansi teknolojia, dini, usafi na uchafu wa mazingira yetu...nguvu na kudhibiti ndio utashi mkubwa wa mwanadamu sasa! (uk. 47)*

Mwandishi anatueleza jinsi wahusika Ndi- na Uledi wanapokuta. Wanasifiana ingawa kila mmoja ana changamoto zake. Ndi- amejitenga na ulimwengu ilhali Uledi naye amesakamwa na ulevi. Uledi anamwambia Ndi- kuwa ana imani naye kuwa hawezi kwisha kwa urahisi kwa sababu anaithamini nafsi yake. Ndi- anatuelezea iliyo falsafa yake:

> *Vipi mtu kama mimi naweza kuithamini nafsi yangu? Mimi niliyekwisha na kumalizika? Lakini kauli yake hiyi ilinikumbusha msemo maarufu ya wakati uliopita. 'Afadhali kuwa maskini na kujitegemea kuliko kupita kuombaomba na kuwategemea watu wengine." Sijaweza kuufahamu ukweli wa msemo huu mpaka hii leo. Vipi maskini anaweza kujitegemea? Vipi anaweza kujizuia asiombeombe? Vipi asiye na thamani anaweza kuithamini nafsi yake? (uk. 38)*

Mwandishi anatusimulia mtagusano baina ya Ndi- na bintiye. Mazzungumzo yanayozua msongo wa mawazo na huzuni mwingi. Mwandishi anatuelezea kauli za Ndi- kisha za bintiye:

> Niliuhisi ule uchungu uliomwenda ndani ya damu yake. Ulipwaja ndani ya rojo lake la damu. Ulifanana na uchungu wangu. ...Hata ile elimu uliyoisimamia kidete na kunikandamiza nayo kwa maneno na vitendo ili nifaulu katika hatua yake, sasa imefaa nini? Hizi "A" nilizonazo katika shahada ya kidato cha sita zinasaidia nini? Mwaka wa saba huu sijapata kazi wala nafasi ya kuingia chuo kikuu kwa ukosefu wamalipo na ukweli kwamba mimi ni binti yako. Damu yako. (uk. 105)

Mtima anaelezea baba yake hali ilivyo katika dunia yake geni kupitia barua pepe. Kule amepatwa na msongo wa mawazo na inamlazimu kunywa dawa kuutibu. Mtima anawasilisha jumbe nzito hapa:

> *Isikushughulishe. Kama wewe, lazima nizungumze na nafsi yangu. Ni njia pekee iliyobaki ya kutojimaliza kabisakabisa. Wewe unajua mtu anapofika ukomo huu. Anapoganda. Kwa hivyo, naandika haya machache kabla sijala vidonge vya usingizi kupoza kiherehere changu.*

*Hata hivi nisemavyo nipo katika maruweruwe tu. Mzito kama niliyelewa kasumba. Mwezi wasita sasa, wamegundua naumwa na kiherehere ambacho wao wanakiita "depression'. Kwa nini ukoo wetu uishie hivi? (uk. 118)*

Katika riwaya ya *Chozi La Heri,* Ridhaa anajaribu kukumbuka matukio yaliyomwandama kabla mkasa aliokuwa akiushuhudia. Haya yote yanampitikia akilini mwake. Zilikuwa ishara tosha ya maafa yaliyompata. Mwandishi anatusimulia:

*Anakumbuka kupepesa kwa jicho lake la kulia kwa muda wa wiki mbili mtawalia. Anakumbuka anguko ambalo alianguka sebuleni mwake, ...anakumbuka mavune yaliyouandama mwili wake na kuunyong'onyeza kwa muda ... Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba nyumbani adhuhuri ya juzi ile. Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku ya kiyama. ... Anakumbuka akimwambia Terry, mke wake, "Milio hii ni kama mbiu ya mgambo, huenda kukawa na jambo. (uk. 1-2)*

Mwandishi anatuelezea hali ya mhusika Selume na jinsi alivyojinasua kutoka dhuluma za wakwe zake. Selume wamekuwa majirani na Ridhaa pale kambini walipokuwa wakimbizi. Hali ilipozidi kuwa mbaya na uhusiano baina ya wakwe kumharibikia aliamua kutengana na mumewe na jamaa zake. Ridhaa anasimulia:

*Selume alikuwa mke wa jirani yetu aliyekuwa mpinzani mkubwa wa Mwekevu. Yeye sasa ameondoka kwake kwa sababu ya kuhitilafiana kimsimamo na wakwe zake. Wakweze walidai kuwa yeye alikuwa mwiba ambao ulitishia kuuletea ukoo wao fedheha. Selume alishindwa kuvumilia shutuma hizi, akafunga virago vyake na kutokomea kokote kule. Sasa Selume anajua maana ya udugu. Anahiari hali hii duni badala ya kuishi kwenye kasri la dhuluma la mumewe. (uk. 30)*

Mwandishi anatusimulia kisa cha mwajiri wa Bwana Kangata aliyeitwa Bwana Kiriri. Huyu Bwana aliachwa na mkewe aliyewafuata wanawe kwenda ughaibuni hata kama mumewe alimrai akae naye waondoleane upweke. Mwandishi anatuhadithia:

*Tajiri wake alikufa muda mfupi kutokana na kihoro cha kufilisika na ukiwa aliokuwa ameachiwa na mkewe, Annette, na wanawe amabo walipata kile wazalendo wa kikwetu hukiita Green Card na kuhamia ughaibuni. Juhudi za Kiriri kumshawishi mkewe asimnyime ushirika wa wanawe ziliangukia moyo wa Firauni. Mama mtu ameamua kwamba hapa hapamweki. (uk. 64).*

Mwandishi anatueleza jinsi mhusika Chandachema alivyopitia madhila kwa makao ya muda ya Bwana Tenge na Bi. Kimai. Bwana Tenge alikuwa msherati alifanya wazi watoto wote na mkewe wakishuhudia. Chandachema alivyoona mienendo hiyo kwa miaka mitatu na zaidi aliamua kugura na hata kulala ndani ya michai ili kuepusha akili yake na msongo wa mawazo, ana lengo na azma pindi tu atakapomaliza kusoma ili kuwaokoa binadamu hasa watoto. Chandachema anatusimulia:

*"Mwaka mmoja, miwili, mitatu ...hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za kisaikolojia nilizopata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigo mkubwa kwa wahisani wangu." "...Siku moja nitakuwa mtetezi wa haki za kibinadamu, hususan haki za watoto." (uk. 106-108)*

Mwandishi anatueleza kuwa Dick anasalia na mawazo mengi baada ya kujinasua kutoka ulanguzi wa dawa za kulevya. Mwandishi anasimulia:

*Miaka kumi ya adha na mashaka imepita. Sasa Dick amekomaa. Ilibidi akomae kwani ulimwengu haukuhitaji 'mtoto wa mama', kama alivyozoea kumwambia kijakazi Sauna ambaye alimtosa katika kinamasi hiki cha kulangua dawa za kulevya. Dick amesafirisha maelfu na maelfu ya vifurushi vya dawa hizi. Mwanzoni hakuwa mraibu wa dawa hizi lakini ilibidi ajizoeshe, kwa usalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi ilibidi kuzimeza dawa zenyewe ili kwenda kuzitapika kwenye masoko ughaibuni. (uk. 119-120).*

Ulanguzi wa dawa ulikuwa na adabu kali na ilibidi hata Dick kuzimeza, jambo analolikumbuka kwa huzuni mkuu anapoamua kuasi ulanguzi na kuanza kuuza vifaa vya stima.

### 3.2.2 Masimulizi ya Onyo

Husimulia matokeo ya mwenendo wa sasa wa kijamii au kiteknolojia. Mfumo huu ulitumika kuelezea imani, na mtazamo wa kundi fulani kwa kutumia kiwakilishi. Wasomaji hutafakari tabia na sera za sasa na hatari zake za baadaye. Upinzani na lawama huonyesha kuwa pana mifumo mibaya inayoongoza jamii.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* mwandishi anatuelezea yale aliyoyatarajia Akida baada ya kupewa zawadi yake. Akida anakuwa na mazungumzo na mwanahabari mmoja na kujielezea matamanio yake maishani. Anatuelezea uwajibikaji ulivyopaswa kuzingatiwa ili mijengo iwe bora na kukomesha mauaji ya majengo mabovu. Anasisitiza kuwa ufisadi ndicho kizingiti kikubwa cha usalama wa binadamu. Mazungumzo ni kama yafuatayo:

> *"Nataka kuwa msanifu ujenzi," nikajibu.*
>
> *"Kwa nini?"*
>
> *"Nimehuzunishwa mno na visa vingi vya majengo yaliyoyojengwa na kusanifiwa vibaya katika miji mingi nchini, yakiporomoka na kuwaua watu bure, burebure bila kisa. Ili kuondokeana na tatizo hilo, lazima wawepo wasanifu ujenzi wengi waliobobea katika fani yao."*
>
> *"Nikidhani ufisadi ndio hupelekea kuwepo majengo yasiyofikia viwango vitakiwavyo kujengwa mijini." (uk.49)*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Ndi- anaendelea kumfahamisha Shaib hatari ya ubinafsi. Anaposema:

> *Tete za ubinafsi; mbegu ambayo isiposhughulikiwa, hukua na ikishakua, hujitutumua na kuvunja kuta za matamanio ya kadiri. Hatari ya mwanadamu tokea enzi za azali ni kuiwachia mbegu hiyo ikue pasi na kikomo, pasi na kizuwizi. (uk. 47)*

Mwandishi anatueleza onyo la baba lililolenga bintiye Yungi ambaye dunia ilikuwa imempa muhuri wa uyeye. Hata kama kila mtu alikuwa na vituko vyake, wosia wa kumshauri binti yake ulimjia akilini Ndi-:

> *Mimi nafahamu, niliwaza. Nafahamu Yungi. Wallahi nafahamu. Labda wewe hufahamu. Ndiyo, mwili ni wako. Una haki nao. Una uhuru wa kufanya upendavyo. Lakini wakati mwingine mwili ni silaha pekee aliyonayo mtu. Sharti autumie vizuri. Sharti aulinde. Mara nyingi mwili unapokuja kudokolewa na kuendelea kumegwa udohoudoho, mtu huwa ameshapotezautulivu wa mwili na akili na kwa hivyo ameshapoteza kila kitu. Ni bora kubaki na kitu, kimoja tu kama roho, kuliko kukosa kila kitu! (uk. 107).*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* Ridhaa anakumbuka jinsi alivyokuwa mmoja wa waathiriwa wa mfumo mpya wa umiliki wa ardhi. Hata shuleni alitengwa na wanafunzi wenzake na kuitwa "Mfuata Mvua." Alipomwambia mama yake kuhusu ubaguzi huu shuleni, mama alimshauri, "Mwanangu, ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba." (uk. 10-11) Ushauri wa mama mzazi ukamwandama kumwamini kila mtu baadaye asije jua wangemchomea aila yake kwa nyumba.

Mwandishi anatuonya kupitia hotuba ya Apondi kuhusu kuthamini maisha na athari za mambo hasi katika usalama wa wananchi. Usalama udumishwe barabarani, katika kampeni na kila wakati haki itekelezwe. Apondi alihutubu:

> *"Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea, inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe, na baadaye wanagawanya ngawira nao! Wengine wetu tumeyaacha magari makuukuu barabarani, kisa na maana, wenye magari haya ni miamba isiyogusika. Wengine nasi tumeshindwa kabisa kudhibiti hasira zetu. Ufyatuaji ovyo wa risasi umesababisha vifo vya wananchi wasio na hatia. Watetezi wa haki wanalilia kile wanachokiita Untimely deaths of innocent people, many of whom are youth. Kumbukeni kwamba hata mtu akiwa mhalifu, ana haki, ana haki ya kufikishwa mahakamani na kushtakiwa kabla hajapewa adhabu yoyote. Kwa hayo machache nawasihi nyote tuungane ili kudumisha amani na usalama nchini mwetu." (uk. 114).*

### 3.2.3. Mtazamo wa Kifalsafa

Maswali ya kimsingi ya kifalsafa kama vile uhuru wa hiari, asili ya mamlaka na maana ya ubinadamu hujibiwa katika riwaya hizi za distopia. uhuru wa mtu binafsi na mahitaji ya kijamii huwekwa wazi. Jamii hukabili hali yao kama hali halisi, bila kupinga wala kuunga mkono.

Katika *Kufa Kuzikana,* Akida anakumbuka vilima Tungule kwa hisia nzito. Katika vilima hivyo takriban miaka kumi ndipo alipofia mama yake mzazi, "Waliosema, 'wakati ni dawa,' hawakusibu. ...Ni hapa Tungule ndipo ulipofia." (uk. 1). Hata baada ya maafa haya, maisha yamemwangazia nyota ya jaha, leo hii Akida alikuwa akienda jiji kuu la Kiwachema sio kuzuru tu bali kuzawadiwa kwa kuupasi mtihani wake na kuwa mmoja wa washindi watatu bora Kiwachema. Leo hii Akida aliiona kuwa wakati ni dawa kwake hata baada ya mauko ya mzazi wake hata vilima vya Tungule hakuwa anavikumbuka maana alipoambiwa tunasimuliwa kuwa hilo jina halikuwa geni kwake.

Akida anatengana na Tim rafikiye aliyegura kuelekea jiji la Tandika. Hata hivyo, bahati inamwangukia Akida anapofaulu mtihani wa shule ya msingi na kualikwa ili azawadiwe na wenziwe wawili jijini Tandika. Hata hivyo safari hiyo inaibua sifa za sekta mbili ambazo hazikuwa zimemfanyia haki babake Akida. Anampa Akida kibarua cha kusaka ukweli kwa sababu hata yeye alikuwa amevimba miguu, sijui kwa matende au maradhi yepi? Mwandishi anatudondolea mazungumzo baina ya baba na mwanaye Akida anatueleza:

> *"Alhamdulilahi! Mungu ni Mkubwa!" Alishukuru babangu. "Basi hima nenda mwanangu Akida wala usikawie. Rehema imefungua milango usilimatie kuingia."*
>
> *"Nenda ofisi ya Kampuni ya Mawakili ya Gembo na wenzake, "...Muulize Bwana Gembo madai ya malipo ya bima ya hayati mamako yamefikia wapi?"*
>
> *"Naam baba nikaitikia."*
>
> *"Tafuta ofisi ya Hatubagui Publishers",..."Kaniulizie mhariri wa Kiswahili, au meneja ya uchapishaji wakefikia uamuzi gani kuhusu mswada wa diwani yangu. Waulize kwa nini wanakawia na miswada ya watu hivyo. Nitakufa jamani bila kukiona kitabu changu cha mashairi kwenye chapa? (uk. 10-11)*

Safari ya Akida ilikuwa inaibua masuala mengi ya maisha. Tangu mamake Akida afe bima waliyoitarajia hawakuwa wamefidiwa. Pili, mswada wake kampuni ya uchapishaji ulikawia pia kutolewa nakala. Tatu, safari hii haikuwa ya kumsabahi rafikiye bali kuzawadiwa. Akida, aliyekuwa na miaka chini ya kumi na tano aliifunga safari hio sio kwa hiari lakini ili asije akakosa zawadi yake ya kuupasi mtihani. ...shughuli hizo zilinielemea kama mizigo mitatu mizito (uk. 11).

Jijini Tandika Tim anamweleza Akida kuwa "Mwenzangu Jiji ni kinywa cha mamba kilicho wazi tayari kummeza mtu. Lazima utahadhari kabla ya hatari (uk. 17). Hii ni baada yao kutoka mkahawani na kuwapata wanawake wamevalia nusu uchi na wamejibanza pembeni kama chui wanaosubiri kurukia mawindo yao.

Akida na Tima wanaposikiza habari kutoka televisheni wanapata habari za kutisha kuwa kwao Baraki kulikuwa kumezuka vita. Tim anamdadisi Akida iwapo alipotoka kijijini kulikuwa shwari au vipi? "Shwari? Pavumapo palilie si kazi kudamirika," Tim alitoa methali na kunyamaza tuli. Kutokana na methali hii Tim anaamini kweli kuwa huenda hali si shwari Baraki. Ishara ya Waziri kukataa na kushutumu magazeti ni ishara wazi kule si kwema. Tim anaeleza zaidi kuwa: "Meno ya mbwa hayaumani" akiashiria kuwa Wakorosho na Wakanju kamwe hawatasikizana. Akida akijituliza kwa kusema; "Sahani zikiwa kwenye treya haizachi kugongana." Alisema haya asije akaharibu ukarimu wa Tim kuwa mwenyeji wake. (uk. 29-30). Tim na Akida wanapoendelea kupata habari, Akida alifaulu kunasa idhaa ya Kiswahili ya BBC London na kupata msomaji wa habari akisema:

> *"Mwandishi wa BBC njini Tandika ameripoti kwamba wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema wametiwa mbaroni na polisi kwa kuchapisha habari za vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyozuka Wilayani Korosho. Serikali imepiga marufuku waandishi wa habari ndani na nje ya taifa hilo la Kiafrika kuingia eneo la Korosho. Mashirika ya kutoa misaada kwa wahasiriwa wa vita hivyo ndio pekee wanaoruhusiwa kuingia eneo hilo."(uk. 30)*

Habari hizi za kimataifa kiliwatia Akida na Tim kiwewe. Likasalie dua ili wazee wao waliobaki Baraki watanusurika athari za vita hivyo vya kikabila.

Akida anapofika jijini Tandika, keshoye anaakia kununua gazeti na anapopotea njia anaamua kupumzika katika bustani moja kabla ya kuendelea kusaka njia hadi kwa mwenyeji wake. Usingizi unamsakama na analala unono. Anapoamka anapata kuwa ameibiwa viatu vyake na wanajiji. Akida alitambua kweli kuwa: Chaka la simba halilali nguruwe (uk. 33). Yeye kuwa mgeni jijini lazima afunzwe na wenyeji kina Ninja. Jioni hiyo Akida aliporejea kwake Tim baada ya kuelekezwa na dada mmoja njia, alifika miguu mitupu ndiposa alimweleza Tim masaibu yaliyompata. Tim alimjibu kifilosofia: "Umepata ubatizo wa Jiji,". (uk. 35). Hii ina maana kuwa sasa anaweza kuelezea maovu yaliyoshamiri jijini kama wizi na kadhalika.

Mwandishi anatusimulia kuhusu Bwana Sululu kupitia mwanawe kumbukizi Akida. Anatueleza:

> Baba alikuwa kafaulu kutenda kilichowashinda hata baadhi ya wanachuo, licha ya kisomo chake haba. Ari na bidii yake havikwenda bure yao. Subira yake ilivuta heri. Nilikumbukia alivyojiendeleza mwenyewe kimasomo baada ya kuhitimu elimu ya ngumbaru. Nikafikia hitimisho kuwa nia ni nguzo muhimu katika maisha ya binadamu, humkokota mtu ikamfikisha kusikotarajiwa katu. (uk. 53)

Nia ya baba kuwa mwandishi ilitimia hata kama ni baada ya miaka kumi. Walichapisha mashairi yake na kuweka nakala kabatini, mwanzo Meneja akituhumu wafanyakazi wa posta ilhali vitabu vilikuwa kabatini.

Tim, Akida na Tamari wanajituma kutafuta riziki. Wanatuthibitishia filosofia kuwa; Mkata hana kinyongo ajapoaswa. Hata hivyo kazi zenyewe ni za sulubu na wakati mwingine za aibu kuu. Akida na Tamari wanasimulia:

> *Tim na mimi tukirauka kila alfajiri kwenda kukoroga zege, kuchimba mitaro, kubeba magunia ya mazao, kusukuma rukwama, kufanya utopasi na kadhalika. Tamari naye aliwafulia matajiri nguo majumbani mwao au kuwapigia deki. ..."Kuoshea mtu nguo kama hizo – hata akiwa tajiri – ni sawa na kuuma jongoo kwa meno hasa". (uk. 119)*

Mtaa wa Falkland uliongozwa na falsafa ya 'kufanya lolote ili kupata chochote. Wengi wa wakazi waliweza kupokonya, kupoka, kupiga pute, kupiga kabari, kukwepua, kuvunja nyumba na kuua (uk. 120), almuradi apate riziki.

Tim anajaribu kubadilisha mtazamo wa vijana wenzake kuhusu kisasi. Tim aliye Mkorosho anawaonya vijana dhidi ya kulipiza kisasi. Vijana wanne walijitoma kwake Tim kumtafuta Akida aliye Mkanju, wakimtafuta ili wamuue kwa sababu alikuwa amemjeruhi baba yao kimakosa na sasa mahaka ilikuwa imemwachilia Akida. Tim anachukua nafasi hii kujaribu kuwabadilisha mtazamo kuhusu ukabila. Anawaaambia:

> *"Umeona wapi kisasi kimejenga nchi?" Tim aliuliza. (uk. 204)*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mwandishi anaonyesha msimamo wake kuhusu athari za ubinafsi. Mtima, alienda ugahibuni na anajaribu kumweleza babake mambo yalivyo kupitia barua pepe. Maisha kule yamejaa ubinafsi na kila mtu anajishughulisha na yake bila kumjali mwenzake. Hali hii inabainika wazi katika usemi wa Mtima:

> *...sina budi lakini kung'ang'ania. Ndivyo maisha ya huku yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake. Kila mtu hujitakia mwenyewe, hamtaki mwingine. Ikizidi dakika moja ya kuwekwa na mtu, basi balaa...Lakini utafanyaje unapokuwa huna pahala pengine pa kwenda? (uk. 7).*

Masimulizi ya Ndi- kuhusu mustakabali wa elimu yanaonyesha kuwa elimu imebadilika. Enzi zake za kupata udhamini na kuhitimu kutoka Makerere College na digrii ya kwanza sio za sasa. Ndi anatueleza:

> *Wakati ule, si leo, elimu ilikuwa ngazi ya kupanda kwendea maisha ya kipato. Angalau kipato wastani cha kujitosheleza. Mimi, nilipokumbuka nguvu za wazazi wangu na mjomba Omari, nilikuwa tayari kujisabilia kwa yote kupata elimu. Aaaa, leo hata mtoto mchanga anajua kwamba elimu ni upuzi mtupu. (uk. 15).*

Mwandishi anatueleza jinsi mhusika Ndi- ameamua kutojishengesha na mambo ya watu; nilijifunza kuepuka mambo ya watu siku hizi baada ya kukumbwa na balaa mara nyingi nilipofanya maamuzi. (uk. 33).

Mwandishi, Ndi anamsimulia mwenzake Shaib kuhusu hali ya sasa ilivyo hasa watawala na watawaliwa. Anasimulia:

*Siku hizi kusema kweli ulimwengu hautawaliwi kamwe na wenye akili. Wenye nguvu za utawala, si wenye akili tena, ni wenye mali na pesa na nguvu za kijeshi. Hao ndio wanaohodhi utaratibu wa maisha, nyenzo za mawasiliano, elimu, sayansi teknolojia, dini, usafi na uchafu wa mazingira yetu. Aaaa, ni nguvu, nguvu na kudhibiti ndio utashi mkubwa wa mwanadamu sasa! (uk. 47).*

Nguvu inayoendesha dunia ni mali na pesa na wasio navyo hawana udhibiti wowote. Mali na pesa vimetumika kama vidhibiti vya kiuchumi na kuonyesha jinsi dunia imekuwa mbaya kwa binadamu.

Ndi- aliporejesha akili zake urazini alijiona kama nyumba yake ndiyo iliyokuwa ikinuka sana kuliko yoyote pale mtaani. Ndi- akajithibitishia filosofia ya waja. Anatusimulia:

*Hasa Bwana Ndera ndiye aliyemcheka kicheko kikubwa zaidi kwangu. Alitunga wivu wa ajabu kwangu tokea pale alipoanza kuporomoka kabla ya mimi kumalizika. Tabia ya watu ndivyo zilivyo siku hizi: wivu, chuki, njama, kwendeana kinyume, kuzungukiana mbuyu, kutotakiana heri. ...kisima chake cha pesa kimekauka. (uk. 128 -129).*

Ndi- anatueleza kuwa kwake muziki na dansi vilimpa uhuru fulani na hivyo kushikilia kama filosofia yake. Alituelezea kwa vigezo vifuatavyo alivyoviorodhesha:

*Nilijua kwamba kucheza dansi ni namna fulani ya uhuru. Uhuru wa kujieleza. Uhuru wa kujieleza bila fujo. Uhuru wenye nidhamu. Sio uhuru wa fujo tu. Muziki na nafasi ya kujijua wewe nani, una uzuri gani, una dosari gani, una uwezo gani. Nafasi ya kufuata urari wa mapigo ya ngoma. ...Uhuru wa kujieleza, uhuru wa urari wa kila kitu. ...Uhuru wa kujieleza kwa kila raia, bila ya kizuwizi. (uk. 162-163).*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* matukio ya kiajabuajabu yalikuwa yametendeka kwake Ridhaa na zilikuwa ishara za ushirikina. Hata hivyo Ridhaa na mkewe Terry wanabadilishana kauli zilizoonyesha msimamo na hatima kuhusu maisha. Mwisho wa wiki hizo mbili janga lilimpata Ridhaa. Nyumba yake ilichomeka na mkewe Terry, bintiye Tila, mkaza mwana na mjukuu wakafa. Mwandishi anatusimulia msimamo huo:

*"si wewe unayeniambia kila mara kwamba hata mtu akijitia wasiwasi vipi, hawezi kuongezea hata pima moja katika maisha yake," akaendelea Terry, "kwamba liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man changed her destiny?" alimalizia Terry ambaye alipenda kuchanganya ndimi alipozungumza. (uk. 2)*

Mwandishi anatuelezea jinsi Ridhaa alivyobaguliwa shuleni kuwa yeye ni Mfuata Mvua, aliudhika na kuapa kuwa hangerudi shuleni tena. Hata hivyo, baada ya ushauri wa mama na kumuasa na filosofia yake: Elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo wala si fujo na chuki (uk. 11). Ridhaa alienda shuleni na kusoma na akaupasi mtihani wake na sasa ni daktari. Lakini kinyongo cha wenzake kilikuja kumletea hasara ya maafa ya aila yake isipokuwa Mwangeka.

Ridhaa anatueleza mtazamo wake wa maisha. Hii ni baada ya kujipata katika makambi na wasiokuwa nacho pia. Tofauti ipo kwa mambo kadha wa kadha kama vile; mandhari ya kifo, hali yao ya kiuchumi na kulipia matibabu, wafu wa vyumba vya wagonjwa mahututi, walevi chakari, mitindo ya mazishi na majeneza ya wafu. Ridhaa anaeleza ambacho ni sawa kwa wote iwapo mauko yatamfika mtu. Anasema, 'Usawa ulio kati ya maiti ni kwamba wote huhojiwa na Munkari.' (uk. 15)

Ridhaa anamweleza mwanawe Mwangeka kwa nini hakuzika majivu ya mama yake, mkaza mwana na wanuna wake. Filosofia yake ya jinsi ya kuwaomboleza wapendwa na lengo kuu hasa ni kupona polepole kiakili. Mwandishi anatusimulia:

*"... Ni muhimu pia ujue kwamba ikiwa unataka kujiokoa au kuzoea hali mbaya inayokukabili ni muhimu kujiingiza katika hali yenyewe, ukaikabili vilivyo ili uache kuiogopa, au iache kukuathiri vibaya. Hii ndiyo sababu nikapaacha mahali hapa jinsi palivyo licha ya rai za jamaa na marafiki kupabadilisha. Najua huenda usiyaelewe haya. Hata hivyo, ishi, utakuja kuyatambua kijana," akasema Ridhaa. (uk. 52).*

Mwandishi anatusimulia yake Mwanaheri na mkondo wa maisha ambao ameufuata baada ya mama yao kuwatelekeza na wao kubakwa awali. Mwanaheri anaona kungekuwa afadhali kwa maisha yao mama yake angetafuta mbinu ya kusuluhisha mgogoro na wakwe na yeye na mnuna mwenzake hawangetaabika. Sasa ana mtazamo tofauti kuhusu maisha. Mwanaheri alisimulia wenzake:

> *"hujiuliza kwa nini mama alitekeleza kitendo hiki cha kibinafsi. Lakini huja nikamlaani shetani kwa kujishughulisha na mambo ambayo siwezi kuyabadilisha. Vipi binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika? Nimeamua kufuata ushauri wa Mwalimu Dhahabu wa kuandama elimu kama nyenzo ya kuniwezesha kuleta mabadiliko katika jamii. Kama mama yangu angetafuta mikakati bora ya kuhusiana na wakwe zake badala ya kukata tamaa, kuukebehi utu wake kwa kututelekeza, na kujikabidhi kwa mauti, huenda maisha yangu na ya ndugu yangu yangekuwa bora zaidi. Kulelewa na mzazi mmoja kuna kero, hasa ikiwa mzazi huyo anaandamwa na majuto daima." (uk. 97-98).*

## 4.0 Mashaka Juu ya Teknolojia na Utandawazi

Teknolojia hutumiwa kama chombo cha ukandamizaji au udhibiti wa maisha ya watu. Maendeleo ya teknolojia yanavuruga maadili ya binadamu na kuleta matabaka mapya ya kijamii. Utu na uhuru wa binadamu hupotea kwa kuwepo na mifumo ya ufuatiliaji. Mgongano kati ya teknolojia na binadamu ni wazi ambapo jamii huingiliwa na viumbe vya kigeni na kupoteza faragha na uhuru wao.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mwandishi anatueleza athari ya teknolojia na sayansi kwa maisha ya binadamu katika dunia yao:

> *Lazima kuuzuia mtutumko...Ni vigumu, si rahisi kamwe...ubinafsi umekuja kuimarishwa na nguvu mno katika karne hii. Nguvu za sayansi na teknolojia ambazo nazo zimekuza utashi wa pesa. Siku hizi vitu hivi ndivyo ishara inayosimamia uwambangoma wa hali ya juu.... Mbele ya ubinafsi, sayansi, teknolojia na utashi wa pesa sisi ni ombwe tupu. ...Ndivyo vinavyotawala hivi leo – sayansi, teknolojia na utashi wa pesa ndio msingi wa dini yetu mpya. Ndizo nguvu zinazotamba hivi leo....Kasi imekwenda mbele mno kiasi kwamba inaonekana kama kwamba hakuna njia ya kuzuia wimbi la uharibifu wake. ...utamaduni tusoutaka hatuwezi kuuzuia tena. Unakuja kama mawimbi yenye nguvu. Ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi ya kuchekesha na miili yetu inajazwa sumu. (uk. 48).*

Maafa ya Bori, mwanawe Ndi- yanatokana na uchu wa kupenda vitu vya stima, kuvirekebisha. Bahati mbaya siku moja shughuli hiyo inabadilika na kuwa karaha. Ndi- anakuja kumaizi baadaye tu kuwa Bori alichukuliwa na umeme aliokuwa akiuchezea. Bori akawa mhanga wa teknolojia ya kisasa aliyoipenda pasi na kuijua. (uk. 152)

Uwanja wa kago ulijaa chuma zilizotupwa za vitu mbalimbali. Hii ni kuonyesha kuwa baada ya matumizi ya vyombo hivi vya kiteknolojia, Waafrika lao ni kurundika mahali vinapoharibika na vinaozea na kuwa hali ya kuleta madhara kwa wananchi. Eti Waafrika tunajua kutumia teknolojia tu! (uk. 188). Mwandishi anatueleza:

> *Hatua baada ya hatua ...kulikuwa na mabaki ya chuma. Hapa mabaki ya chuma ya melinyangumi. Pale mabaki ya chuma ya trenikiwaviwavi. Mbele zaidi mabaki ya chuma ya matrendovu. Kushoto mabaki ya chuma ya sagamaweboko. Kulia mabaki ya chuma ya simbamwene. Chuma winjifaru. Chuma magarinyati, makubwa na madogo. Chuma mashinenge. Vyuma vimekuja kutupwa ovyo kutoka mbali. Na mbele zaidi mabaki ya madawa ya sumu amabyo yalihanikiza harufu iliyowaendesha chafya watu kila mara. (uk. 187).*

Ndi- anatuelezea athari ya utandawazi na teknolojia katika maisha ya binadamu. Anaiita ki-Ungu. Hili ni angamizo kubwa sio kwa maadili bali kunyambua na kufisha misingi yote ya ulimwengu. Anatueleza:

> *Globalization mara Americanization. Na lilipotimka lilitifua kila kitu dhaifu katika kasi na mikiki yake. Kila kitu kilipojaribu kufukuzana nalo, kilijikuta kinawachwa nyuma milioni ya kilomita. Likapita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likiripuka mandimi ya moto yaliyounguza na kukausha kila kitu: watu, wanyama, barabara, majumba, miji na majiji, mashamba, mazao ya chakula, mazao ya mauzo, miti, maji, hewa, pwani, bahari, nchi kavu, madini, umeme, mafuta, hospitali, madawa, benki, viwanda, biashara, rasilimali zote ... shule, vyuo, desturi, mila, tamaduni na hata uhai, heshima na mustakabali wa watu – hata roho zao. Lilipenya hata ndani ya nyumba na vibanda vya watu na kusasambura na kupekua kila kitu, kukashifu na kufedhehi na kisha kuangamiza lilivyopenda. Lilingia humo na kutawala na kuamrisha na kulazimisha mambo katika nyumba yake mwenyewe mtu. (uk. 206).*

Katika *Chozi La Heri,* Dick anasimulia jinsi teknoljia ilivyomumulika na nyenzo alizotumia kuipiku teknoljia yenyewe ili aweze kufanikiwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya. Anasema:

*Dick amesafirisha maelfu na maelfu ya vifurushi vya dawa hizi. Mwanzoni hakuwa mraibu wa dawa hizi lakini ilibidi ajizoeshe, kwa usalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi ilibidi kuzimeza dawa zenyewe ili kwenda kuzitapika kwenye masoko ughaibuni. Hili lilitokea wakati mashine za forodha zilipopata makali zaidi siku nyingine na kung'amua shehena ambazo zilikuwa zimeshonewa kibindoni. (uk. 120).*

Ilimbidi Dick kumeza dawa na kuzitapika ughaibuni.

### 4.1. Mtazamo wa Baada ya Maangamizi

Binadamu wanajijenga vipi baada ya kuanguka? Wahusika wanajiinua vipi baada ya mikasa na changamoto? Mtazamo huu huelezea matumaini ya mabadiliko na mustakabali bora. Juhudi huwepo za kujaribu kuondoa mifumo mibaya ya distopia.

Katika *Kufa Kuzikana,* Tom Mangala alioa Mzungu baada ya kumaliza masomo yake ya Uzamili Marekani. Wana ndoa hawa wawili wakaamua wasizae mtoto. Kufidia ukosefu wa mtoto tunamwona Mzungu huyu akilea mbwa. Mwandishi anatuelezea:

*"...akajibu huku amekipakata kijibwa chake cheusi kama kitoto. Wazungu nao na vinyama vipenzi vyao! Kwetu kupakata mbwa na kumbusubusu kama alivyokuwa akifanya Jenelle huonwa kama uchizi au mahepe (uk. 84).*

Jerumani aliyekuwa akisomea Ujerumani, kama mhusika Tom anarudi kwao maisha yanapomwendea mrama na kuanza kuchotea watu maji kwa mkokoteni. Anapoulizwa kuwa haoni aibu kukokota rukwama, alikuwa na mtazamo mzuri wa maisha. Anasema:

*Aibu ya nini? Mimi si bwana mkubwa wa watu hao wa Sangura. Mimi ni mtumishi ati. Nimeona Ujerumani matopasi na wafagiziwakizifanya kazi zao kwa kujituma. Ndivyo maana tunapaswa kufumua mioyo yetu na kuifuma upya. Hiyo ndiyo siri ya maendeleo. (uk. 156)*

Kabla Akida kugura Kiwachema kwa ufadhili wa Tom nchini Canada alisikia redio ikitangaza kuwa serikali ingebuni Tume ya Haki na Maridhiano kuhusiana na vita vya kikabila Wilayani Korosho. Zaidi idhaa ilisema kuwa Mheshimiwa Mabende kauwawa na afkani mmoja jina lake Johnstone Muyaka. Mauaji aliyatekeleza kwa kutumia bunduki ya baba yake katika sehemu ya Binge, Wilayani Sangura. Tetesi zilikuwepo kuwa muuaji katorokea nchi jirani. Hizi ni harakati za kusuluhisha maovu yaliyokuwa wakiendelea Kiwachema.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatusimulia hatua ambazo Mwangeka alichukua baada ya kurejea kwao na kukumbana na hasara ya vifo vya mkewe, mwanawe, mama yake na wanuna wake. Anasema:

*Mwangeka hakuishi na baba yake kwa muda mrefu baada ya kurejea kwake. Kwanza, hakuweza kustahimili uchungu uliosababishwa na kuamka asubuhi kutazama mahali ilipoangamia aila yake. Kila siku alimshawishi baba yake akabomoe kiunzi kile cha nyumba, naye baba mtu alikataa katakata. Alishikilia kuwa hilo ndilo kaburi la ukumbusho wa familia yake. Pili, ilibidi Mwangeka ayaanze maisha yake upya, atafute mbinu ya kumwezesha kukabiliana na hali yake ya ukiwa. Atafute ushauri kutoka kwa wataalamu, auuguzie moyo wake mbali na babake. (uk. 57).*

Mwandishi anatuelezea maisha ya Naomi baada ya kumtoroka mumewe na wanawe. Baadaye Naomi aliajiriwa na Kimbaumbau na kudhulumiwa kwa nia fiche ya kufanya ufuska naye. Baadaye Naomi anajuta alipoenda kuwatafuta wanawe Mlima wa Simba na kuwakosa lakini akapata kaburi la mumewe kuliko mahame. Naomi anajirudi na kujiajiri kwa kujifungulia kiafisi kidogo karibu na Chuo Kikuu cha Mbalamwezi. Kule anawapigia wasomi kazi zao chapa na kuisarifu miswada yao. Hata hivyo ni mwingi wa huzuni na majuto, "Maskini wanangu, huenda tusikutane nikiwa hai, ila nawausia kwa kauli moja tu, msiache ubinafsi na tamaa kuupweza ubinadamu wenu." (uk. 193)

### 4.1.2. Mtazamo wa Kiuchumi/Kinyume na Utopia

Jitihada za kutafuta jamii bora zinaweza kuzaa matokeo mabaya yasiyotabirika. Tamaduni za asili hufutwa au zilikandamiza mila na desturi za watu ili kudhibiti fikra na tabia zao. Serikali au mamlaka zilitumia nguvu zao kuzuia utambulisho wa watu na kuwafanya kuwa sehemu ya mfumo mmoja wenye malengo maalum. Biashara na ajira huwa sekta kuu za kuleta maangamizi.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* mashamba ya akina Akida na Tim yanapakana. Hata Tim anaeleza kuwa kila mwaka shamba la akina Akida linanapata mazao bora kuliko lao. "Lakini shamba lenu lina rutuba kuliko letu." Hata ng'ombe wenu wanatoa maziwa mengi zaidi. Mambo yenu yanatengemaa kila mara... (uk. 13).

Tim anakusudia kusema kuwa mazingira kwao Akida yana fanaka fulani kushinda kwao. Anazidi kuelezea sifa za babake Akida ambazo labda ndizo anafungamanisha na baraka kwao shambani. "Na babako pale alipo, jirani mpole na mwenye moyo mweupe. Hana neno na mtu. Lini watu watakapoanza kuuona ubaya au uzuri wa mtu bila kuvaa miwani ya ukabila?" (uk. 15)

Tom Mangala aliwakodi askari kwa kuwalipa hela nyingi ili wamsindikishe na rafikize Baraki kumzika Mzee wake Mangala. Tom asingekuwa na uwezo wa kuwalipa askari hangeweza kwenda Baraki na kumzika Mzee wake. Akida anatusimulia:

Askari wote watatu walikuwa katika hali ya tahadhari kutulinda dhidi ya uvamizi wowote. Tom alikuwa amewakodi kwa kiasi kikubwa cha pesa kuja kuhakikisha kuwa Mzee Mangala anazikwa salama mahali alipotaka mwenyewe baba mtu alipokuwa yu hai.

Tim alipozidiwa na madeni baada ya kufutwa kazi ilibidi auze hadi TV na gitaa na hata kugura makazi hadi Mtaa wa Falkland. Akida anaporejea Jijini baada ya kumsindikiza Tom kumzika Mzee Mangala anakumbana na mapambano ya kiuchumi. Akida na Tim walikuwa na mazungumzo yafuatayo:

> *"...Vitu umevipeleka wapi?" "Nimeviuza"*
>
> *"Hata TV na gitaa?" "Karibu kila kitu, hata viti, redio na baadhi ya nguo. Nikipata kazi nyingine n'tavinunua vingine. Nilikuwa na madeni ambayo ilikuwa lazima kuyalipa... Samahani hata nakala zote za Kero za Mkiwa nimeziuza...."*
>
> *"Si, hoja bwana, hata ingawa sikuwa nimeisoma nakala yangu." (uk. 112)*

Mkewe Tom, Jenelle alipopokea ujumbe kuwa mumewe kanusurika kifo, alirejea Tandika na kumchukua mumewe Canada kwa matibabu. Akida na Tim walikuwa wameenda kumtembelea na kumkosa hospitalini wakidhani 'ameenda' iliashiria kifo – mwili umepelekwa nyumba ya maiti. Hata hivyo mgonjwa mmoja aliyelazwa pale hospitalini aliwafafanulia 'kuenda':

> *"Nyie nanyi mna mambo," ..."Hamuelewi?" Yule amekwenda ng'ambo. Mke wake Mzungu amekuja hapa jana zimempanda za kwao. Amempeleka sijui Canada, sijui wapi kwa matibabu. Heri wenye wake Wazungu. Sisi wengine tutajifia hapa burebure. Madaktari wa kwetu wanazembea tu. Ee! Dau la mnyonge halendi joshi (uk. 123-124).*

Uwezo wa Jenelle ulionekana kama kigezo cha uwezo wa kiuchumi kumwopoa mumewe kutoka hospitali wasiwasi za Kiwachema.

Akida na Tim waling'ang'ana na maisha magumu pale Mtaa wa Falkland, hawakuweza kujikwamua kutoka tope la ulitima walimokuwa wamekwama. Lakini wenzao wenye hali waliendelea na maisha yao kama kawaida. Akida anaelezea:

> *Uhaba wa bidhaa muhimu ulianza taratibu kushamiri Jijini Tandika, tukaanza kuzipiga foleni madukani. Vitu vya kawaida kama vile majani ya chai, chumvi na sabuni vikaadimika kama wali wa daku. Bidhaa kama sukari, maziwa na mkate tukaziondoa kwenye orodha ya mahitaji ya kimsingi. Hivyo vikawa vitu vya starehe isiyokuwa ya lazima na tusiyoweza kuimudu. Dau la mnyonge haliendi joshi. Bila shaka wenye nafasi zao za hali walizimudu starehe hizo. Lakini hao hawakuwa wenzetu. (uk. 127)*

Akida anapomuua mtu anayekisia alikuwa Mzee Zablon anaamua kukimbia kwenda Sangura. Alipoingia basini, wachuuzi waliuza bidhaa zao kwa masharti na hivyo kuwahadaa wateja wao. Akida anasimulia aliyoshuhudia baadaye maana mzee yule aliuziwa kipande kidogo sana cha kitambaa kilichofungwafungwa vizuri kwenye kipande cha katoni. Kumbe wachuuzi Tandika Jijini wana akili tendaji sana. Akida anatueleza:

> *Mzee mmoja aliyekuwa amekaa karibu nami alishawishika kununua kitambaa cheusi cha kushonea suti. Kilikuwa kimekunjwa vizuri, wala mchuuzi hakumruhusu kukikunjua. Mama mwingine akanunua tochi ya betri zake kutoka kwa mchuuzi mwingine ambaye pia alitoka kasi punde baada ya kupokea pesa. Kijana mwingine akanunua saa ya mkono na muuzaji akatoweka punde....Kupiga bei kwa chochote ni kitambulisho cha watu wa nchini kwetu Kiwachema. (uk. 134-135)*

Akida alipokimbia Jiji la Tandika alishuka njiani eneo la Binge. Hapo Binge alikumbuka kuwa kulikuwa na mchuuzi aliyeitwa James. James aliuza bidhaa kwa masharti. Akida anatueleza:

*Anawauzia watu sukari kilo mojamoja....Tena ukinunua sukari unaambiwa lazima ununue pia maziwa ya ungaunga ilhali huku shamba wenyewe tuna ng'ombe wa maziwa tele. Ukitaka sabuni unaambiwa sharti ununue karatasi ya shashi na sisi huku majani ya miti yanatosha (uk. 146).*

Hali ngumu ya kiuchumi ilimulikwa na Jarida la Jerumani. Jarida hili lilikuwa limechapishwa na shirika moja la kutetea haki za binadamu. Lilieleza:

*Wafadhili wamezuia misaada na kuongeza msumari wa moto kwenye donda. Uchumi umevia, na unatarajiwa kudidimia zaidi. Upo mfumko wa bei na uhaba wa bidhaa kila mahali Kiwachema. Mishahara nayo imekuwa kama maziwa ya kuku, muhali kupatikana. Walimu hawana mishahara. Wafanyakazi wa mabarazaya miji hawaijui rangi ya mishahara miezi nenda miezi rudi. Wametelekeza kazi zao ama wanafanya biashara au wanazumbua riziki kwa kuwabughudhi wachuuzi ili wapewe 'kitu kidogo.' (uk. 161).*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Ndi- yu mazungumzo ya akilini na Shaib. Anamweleza masuala ya kiuchumi na jinsi dunia inavyoyafasiri:

*Unapigana kuondoa umaskini wa dunia. 'New World Order, WTO, Globalisation' – kipanya na ndovu wanaposhindana nguvu....Fedha. Fedha. Fedha. Pesa. Pesa. Pesa. Misaada. Misaada. Misaada. Mikopo. Mikopo. Mikopo. Haihatarishi tena uhuru wetu! Kama husujudu unaangamia. Kama huna anayekutetea utafutika kabisa juu ya uso wa dunia. (uk. 46).*

Ndi- anasimulia safari waliyopelekwa na Wajapani ili kuwaweka vijana wa dunia pamoja wafahamiane. Safari ya miezi mbili ilimpa maarifa tele na pamoja kushuhudia jinsi asasi ya kiuchumi ilivyomenyeka katika kisa kimoja. Anasimulia:

*Lakini dunia hii leo ina maharamia wa aina nyingine, kama vile kwa mfano, wanaonunua dhahabu kwa kulipa asilimia 5 ya mapato yote ya machimbo na kuchukua asilimia 95. Kuna pia wanaouza dhahabu kununua maradhi ya watu wao. Una nyuso ngapi uharamia au wizi? (uk. 96)*

Ndi- anamsimulia kivuli chake Naima, binti mmoja waliyecheza naye akiwa mdogo. Anamweleza athari ya waliogura kwao na kuja Kijiweni. Walitupora raslimali yetu na kutuacha hohehahe. Ndi- anamwelezea Naima:

*Wakajitahidi kuti mikonge yao ya tembo kwenye ardhi hii na kuifyonza nguvu na utajiri wake na kuupitisha mguu mwingine kuneemesha kwao. Na sisi wakati wote huo tumebaki katika mzugo unaotufanya dunia milele! (uk. 98)*

Ndi- anasimulia Mtima maisha ambayo Yungi hujihusisha nayo leo hii. Yungi aliyekuwa kahaba na mvutaji sigara ni kama alighairi nia na kuacha mambo hayo. Baba yake anasema:

*...ingawa nilikuwa na hakika si kazi ya kujiuza na kusabilia watu mwili wake tena. Tuseme kazi za sabaganga alizofanya kutibu maradhi kadha yaliyotukumba. Si kazi moja wala mbili. Mara kafuma foronya na kuziuza. Mara kazitia nywele za wenzake katika chombo fulani kuzitokosa, na zinapoiva alizitoa zikiwa tambi si tambi wala mboga ya mtoriro si mboga ya mtoriro, kisha akawatoza pesa. Mara kasafiri na kurudi na mabunda ya mitumba na kwa muda wa wiki kadha mbele ya mlango wetu palikuwa na duka la nguo kuukuu. Pesa zikaingia mikononi mwake. (uk. 151)*

Utandawazi ulikuwa na athari kubwa kwa mataifa mengi yanayoendelea, hasa ya bara la Afrika. Mwandishi anatuelezea vikwazo vya kiuchumi na madhara ya utegemezi misaada. Anatueleza:

*Sauti lake la ki-Ungu nilisikia likijaa kila pahala: hewani, baharini, ardhini, angani, mwezini, magazetini, simuni, redioni, televisheni, sinema, na kwenye kompyuta...Mara chache nilisikia ikisema kw rehema na kuionelea dunia ya wachochole na kuifunika mwamvuli wa World Bank na IMF. Likasikika likisisitiza haki za binadamu huku lenyewe linapita kuvunja haki za binadamu na kujumuika na wavunja haki za binadamu na walioimarisha maslahi yake....Hata nchi zilipomkasirisha ziliwekewa guu na kubanjwa na kudamirishwa kwa njaa, maradhi na watu. (uk. 206)*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* Ridhaa anakumbuka mazungumzo waliyokuwa na bintiye Tila kuhusu wageni walionyakua ardhi na sasa ndio wanaomiliki nyenzo za uzalishaji. Wageni wamekuja na kuchukua

mashamba yao, wanawapa vibarua vya kijungu jiko wafanye shambani, Waafrika ndio wanunuzi wa mazao yao na waendelee kumwongezea ngawira yake mlowezi. Ridhaa anayakumbuka maneno aliyomwambia Tila, bintiye:

> *"mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria za mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikaji wa ardhi na Waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa ... yote yakapata wenyeji wageni ... dau la Mwafrika likagonga jabali. Waafrika, akiwemo baba, Mzee Msubili, walilazimika kuwa, ama vibarua katika mashamba taliyokuwa yao, au maskwota... (uk. 7)*

Mwandishi anatueleza jinsi hali ya vijana ilivyo. Vijana wakehitimu vyuoni na hawana ajira. Hawawezi kujiajiri kwa kukosa mtaji. Wanashauriwa warudi vijijini wakalime, kule nako vikata ni vidogo au wameporwa. Anaelezea hali tata ya kiuchumi jinsi inawaacha vijana katika njia panda:

> *... Hapa ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu na maelfu ya ekari, wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwamakubwa huku wakidai ni njia ya kuwahakikishia wenyeji hali ya kujitosheleza kwa chakula. Kumbe wanakuja kutufukarisha zaidi! (uk. 21-22).*

Mwandishi anatuelezea zaidi kuhusu uhitaji wa mhusika Kairu na familia yake. Kairu anaelezea hali yao ya kiuchumi na jinsi amekabiliana nayo hadi amefika kidato cha pili. Athari ya mzozo wa maji na samaki uliwakosesha karo ikabidi mama yake Kairu kumlilia mwalimu mkuu ili alipe kidogodogo hadi mwisho wa mwaka, ilhali baba yake mzazi ni mtu aliyenacho – lakini hawezi kumlipia karo maana ni mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa. Kairu aliwasimulia akina Umu wakiwa darasani:

> *"... mimi mzazi wangu wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki, na baada ya ule mzozo wa nani kamiliki Ziwa Kuu, biashara imepigwa na mawimbi makali. Nasikia wavuvi wa humu mwetu wanahofia kuvua huko kwa sababu wameambiwa kuwa japo ardhi ambayo ziwa limesimama ni yao, maji ya ziwa si yao! Hivyo inasemekana kuwa hawafai kuvua huko, kwamba samaki ni ya wanaoyamiliki maji! Matokeo ya mzozo huu yamekuwa masikitiko kwa familia nyingi. Samaki wamekuwa adimu sokoni na bila shaka bei yake inaweza kutabirika. Kwa mtu maskini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzisha biashara nyingine, maisha yamekuwa magumu zaidi." (uk. 92-93).*

Mwandishi anasimulia mtazamo mpya wa Dick baada ya kulangua dawa na kuamua kubadilisha mkondo wa maisha. Anasimulia:

> *Aliacha biashara hii haramu na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya umeme. Sasa ameanza kujitegemea, hakika amejiajiri. Ameamua kufungua ukurasa mpya katika maisha yake. Amekwisha kuhitimu masomo katika chuo cha kiufundi ambako alijifunza Teknolojia ya Mawasiliano ya Simu. Ameweza kuyadhamini masomo yake kwa pesa ambazo alikuwa akidunduiza siku za biashara haramu, na baada ya kujitegemea. Sasa amepanua mawanda yake ya biashara. Anauza vifaa vya simu. Husafiri ng'ambo mara kwa mara kununua bidhaa ili kuyauzia mashirika yanayotoa huduma za mawasiliano. (uk. 124)*

Mwandishi anatuelezea jinsi Dick alivyoimarika kiuchumi baada ya kupata familia iliyomlea baada ya kubadili mkondo wa maisha – anawasifu Mwangeka na mkewe Neema walio pia wazazi walezi wa Mwaliko kaka yake. Dick anasimulia:

> *Tulipokutana nilikuwa na kiduka kimoja tu cha kuuzia vifaa vya simu. Hivi sasa nahesabiwa katika safu ya wanajamii mashuhuri katika kuendeleza TEKNOHAMA.... Biashara yangu hii ya vifaa vya mawasiliano ya kisasa imebuni nafasi nyingi za kazi kwa wanyonge ambao wangekuwa mawindo rahisi kwa wahalifu. (uk. 174)*

## 5. Hitimisho

Utafiti huu ulihakiki riwaya tatu za Kiswahili *Kufa Kuzikana, Dunia Yao* na *Chozi la Heri* na kimahsusi ni kutoa maelezo ya kina hasa yaliyolenga mitazamo ya daistopia yalishughulikiwa barabara. Tuliamua kuhakiki riwaya tatu pamoja kwa sababu zililenga mada yetu ya utafiti sawasawa. Usomi kwa riwaya hizi unaelezea masuala ya daistopia jinsi yanavyoathiri jamii ilhali jamii inaishi kwayo na kujikakamua. Jamii ndani ya riwaya hizo na hasa wahusika waliishi ndani ya hali hiyo ya uozo kutuonyesha kuwa walidhibitiwa na hali hizo.

Riwaya ya *Kufa Kuzikana* ilisawiri wahusika walioishi katika jamii iliyojaa ufisadi, ukabila, uongozi mbaya, matumizi ya pombe, umasikini, fujo na ghasia na hali nyingine nyingi kandamizi kwa maisha ya binadamu. Kwa sababu hiyo, wahusika walionyesha hali ya kutamauka na hali hizo ngumu na kukosa uwezo wa kujiokoa kutokana na hali zao mbaya. Ukabila na machafuko ya kisiasa ndilo jambo kuu lililojitokeza na athari yake katika jamii na mazingira. Vita vya kikabila vilivyochochewa na siasa mbaya husababisha akina Akida kubakia yatima na kubahatisha kimaisha. Asingekuja kukutana na Tom, huenda Akida angebaki maskini hohehahe na kujifia.

Vita hivi vya kikabila, vilisababisha machafuko ya kimazingira, uharibifu wa mijengo na makazi ya binadamu na kusambaratisha familia nyingi sana. Mhusika Tom alimpoteza baba yake mzazi na karibu auwawe na mahasidi waliomuua baba alipoenda kumzika baba yake kijijini kwao. Mwishowe Tom anaamua kutorokea Canada na mkewe kwa sababu nyumbani hakukaliki tena. Rafikiye Akida, Tim naye alihangaika na maisha ya mjini Tandika na kufikia mwisho wa masimulizi mwandishi alituonyesha kuwa bado Tim alikuwa anaishi mtaa duni na maisha pale mjini yakiwa ya kubahatisha tu.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* hali za daistopia zilizosawiriwa katika riwaya hii zimesababishwa na mwandishi kutamaushwa na mustakabali wa bara la Afrika ambalo limezongwa na kila aina ya uozo kuanzia umaskini, uchafuzi wa mazingira, ukoloni mamboleo, ubinafsi, dhuluma dhidi ya binadamu na utandawazi. Mwandishi au msimulizi ametumia mhusika Ndi- kama kielelezo cha kuonyesha kuporomoka kwa bara la Afrika. Matukio yanayoshuhudiwa katika familia ya Ndi- yanalinganishwa na mataifa ya Kiafrika ambayo hupatwa na matatizo yanayotokana na wananchi wenyewe kwa kukosa kujielewa. Aidha wananchi huisahau na kuibeza asili yao huku wakiiga mambo ya kigeni kutoka kwa mataifa yaliyoendelea katika takribani kila nyanja ya kimaendeleo. Kutoshirikiana katika ujenzi wa taifa lao na kutojikomboa kimawazo huzua hali ya wasiwasi na maafa. Kulingana na mwandishi wa riwaya hii matatizo haya yanajitokeza katika uchumi, jamii, siasa na hata dini. Hivi kwamba, Mwafrika analo jukumu la kubadilika na wakati kwa kuzaliwa upya pamoja na jinsi ya kujiendeleza kimaisha.

Utafiti huu umebainisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu baina ya mtindo na daistopia kimaudhui na kimtazamo. Kuzuka kwa utandawazi kumechangia kudhoofika kwa maadili katika jamii ya Kiafrika jambo ambalo limekuza katika muktadha wa kimtindo. Atari za utandawazi zimeshuhudiwa sio tu upande wa kuporomoka kwa maadili, bali hata katika itikadi za kisiasa zilizokopwa kiholela. Mifumo hiyo ya kigeni ya kisiasa inapwaya inapotumiwa katika muktadha wa Kiafrika. Bara la Afrika limekosa utambulisho na kujipata katika njia panda kiitikadi, kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii.

Riwaya hii inasawiri vijana 'dunia yao' yaani ulimwengu wa kifantasia ambamo wanaonekana kutojielewa, kudhibitiwa na nguvu fulani, kuasi asili yao pamoja na kuudharau utamaduni wao. Kutokana na uigaji wa utamaduni wa kimagaharibi, vijana wamekuwa watumwa katika bara la Afrika. hiki ni kinaya kuwa bara la Afrika lilipata uhuru na kujitawala. Baadhi ya vijana wamesawiriwa kama waliopoteza nguzo za utambulisho wao wa Kiafrika baada ya kuangamizwa ki-utamaduni huku maadili yao yakidhoofika kwa kujihusisha na uozo hususan matumizi ya dawa za kulevya, kutowajibika na kutowaheshimu wazee wao jambo ambalo limechangiwa sana na utandawazi. Baadhi wameambukizwa magonjwa ya zinaa na kuishi kutawaliwa na hofu.

Mwandishi huyu ameonyesha jinsi serikali zimedhibiti wananchi wake na kueneza mfumo wa ukandamizaji. Uhuru wa kibinafsi umepotea na unyonyaji wa rasilimali na kudidimizwa kimaendeleo kutokana na mfumo dhalimu wa soko huria. Tamaa ya uongozi, ufisadi, wizi wa kimabavu, ubakaji wa watoto wachanga umehalalishwa.Viongozi wametawaliwa na ubinafsi unaozua matabaka kadhaa. Wananchi wanaonekana kung'ang'ania masalio ya wenye nguvu pamoja na hali zao za umaskini. Vijana wamekosa nafasi za kazi kwa sababu lazima watoe rushwa au wawe na uhusiano wa karibu na wenye vyeo serikalini.

Mohamed anatumia mandhari ya distopia katika kazi yake ili kusudia kutoa tahadhari na pia kutabiri hatari ijayo ya viongozi wasiowajibika, wanaotunga sera zisizostahili na matokeo ya kutodumisha haki za kibinadamu. Athari za ubinafsi na uporomokaji wa familia unadhihirika kutokana na familia ya Ndi-. Woga, udhibiti, kutamauka na uasi ndivyo wahusika wanajihusisha kila uchao angalau waendelee kuishi. Mitazamo iliyolenga mada iliwekwa wazi na kuelezewa kwa kina. Wahusika na mandhari ni vipengele muhimu vilivyochangia kufanikisha upataji wa data yetu ya utafiti.

## Marejeleo

Bibiana, S. (2014). *Trajectories Of Social Isolation.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Cha Indiana. (*Isiyochapishwa*).

Bradford, W. (2003). *Growth of Literature.* London: Kingsway Ltd.

Bryman, A. (2004). *Disneyization of Society*. London: Sage Publication Limited.

Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style.* Paris Librairie: Hatier Publishers

Camus, F. (1984). *The Control of Man's Fate in The Stranger.* London: Salman Ltd.

Chacha, N.C. (1980). Ushairi wa Abdilatif. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Chepkwony, B. (2017). *A Literary Histographical Analysis of Kinyanjui Kombani's: The Last Villians of Molo.* Makala: *African Studies Journal PP 102-116.*

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group Ltd.

Holman, C. H (1960). *A Handbook to Literature* (Revised and Enlarged). Salisbury: The Odyssey Press Inc.

Jackson, P. (1999). *Understanding West Literal works*. Dublin: Ireland Pub. Ltd.

Kehinde, A. (2004). *Post Independence Dissillusionment in Contemporary African Fiction*. Nairobi: Oxford University Press.

Kerlinger, F. (1969). *Research Myths: Statistics, Practicability and Status.* London: Taylor Press.

Kimani, N. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: University Press,

Kimani, N. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai Industries Limited.

Kimani, N. na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kinoti, N. (2012). *Mtazamo wa Mwanasiasa wa Kiafrika Katika Ushairi.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kitula, K. (1999). *Language Development Research in the 21st Century*. Nairobi. JKF.

Kombo, D. & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kruger, (1998). *Usawiri wa Mwanamke Kama Mhusika wa Fasihi*. Makala ya utafiti.

Leech, G & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose.* London and New York: Longman.

Masinde, E. (1992). Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Matei, A. (2014). *Chozi La Heri.* Nairobi: One Planet Publishing & Media Services.

Marx, K. (2004). *Capital* Vol 1, *Afterwood to the Second German Edition*(4). Berlin: AGM.

Merriam, W (2003). *Merriam Webster Collegiate Dictionary.* London: Merriam Webster.

Mohamed, S. (2006 ). *Dunia Yao.* Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd. M. Press

Mugambi, H. (1982). Fasihi yetu. Nairobi: OUP.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Me*thods. Nairobi: Acts Press.

Mutua, J. M. (2017). Mitazamo ya Waandishi wa Kike na Kiume Kuhusu Usawiri wa Wahusika wa Kike

katika Tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Pwani.

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso Katika Jamii ya Watigania. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muhamed, B. (2011). Usemezano kama Mkakati wa Katika Fasihi Andishi. Tasnifu ya Uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mukobwa, F. (1987). Kazi na Faida za Jamii. Nairobi: JKF.

Mungai, M. (2013). *Nairobi's Matatu Men*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Musangi, J. (2008). *A Walk Through the Criminal City*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Witwatersrand. Afrika Kusini: (Haijachapishwa)

Mwanje, I. J. (2001). *Qualitative Research Process: Social Science Research Methodology Series, Module 2*. Addis Ababa: OSSREA

Ndago, G. (2020). *Nationhood and Ethnic Ideology: examining selected Cartoons Paratextsin* Kwani? *Kiswahili.* Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).

Ngolo, E. K. (2011). Mabadiliko ya Kimtindo Katika Ushairi wa Said A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Odhiambo, T. (2004). *(Un)popularity of Popular Literature in Kenya: The case of David Maillu*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Witwatersrand. (Isiyochapishwa). ______(2010). *The Postcolonial City*. Makala mtandaoni.

Oiko, F. (2017). *Uhakiki wa Kimtindo Katika Tamthlia za Arege*. Chuo Kikuu cha Maasai Mara. Tasnifu ya Uzamili. (Iliyochapishwa).

Okwena, S. (2013). Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia za Arege. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Oxford, (1978). *Advanced Dictionary of English.* Oxford: OUP.

Ponera, A. (2019). Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu. Dar es Salaam: CTP.

Said, E. (1978). *Orientalism.* Newyork: Newyork Publishers.

Scholes, K. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction.* New York. YUP.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.-----------(1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaaam: Press and Publicity Centre.

Syambo, K. na Mazrui A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Truex, D. (1996). *Theorizing in Information Systems Research*. Oxford: OUP.

Wafula, R. M. (1987). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: JKF. _____________ (2003*). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers. ______________ (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Limited. ______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uhakiki na Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Woods, J.T. (1997). *Communication Theories In Action.* London: Wadsworth Publishing Company.